SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



UKURASA 3

## KESI YA MBOWE
Shahidi aliyeugua ghafla kizimbani kuendelea leo




# Nipashe
Jumatatui Februari 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580856
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# Sakata Ngorongoro lawagawa wabunge

**SPIKA** aombwa kuunda kamati teule...*Endelea Uk. 2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akipokea maelezo kwa mmoja wa wajasiriamali waliohudhuria hafla ya uzinduzi wa ushirikiano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Benki ya CRDB kupitia mikopo ya wajasiriamali ya 'Inuka na Uchumi wa Buluu'. Kulia ni Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda Zanzibar, Omari Said Shaaban na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kulia). Habari Uk 5. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

UKURASA WA 4

RIPOTI MAALUM

## AITOA SHULE MKIANI NA UHALIFU HADI KUNG'ARA KINIDHAMU

NI simulizi yenye ukakasi kusikia shule ambayo miaka mitatu iliyopita ilikuwa imetawaliwa na matokeo 'divisheni ziro' si chini ya wanafunzi 100 kila mwaka na katika nafasi ya tatu kutoka...

UKURASA WA 5

## MBARONI MADAI KUUA MTUMISHI WA KANISA

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia, Daniel Mwilango (42) kwa tuhuma za kumuua kwa kumkata mapanga, Nickson Myamba (48), aliyekuwa Katibu wa Baraza la Walei la Kanisa...

## Ukame ulivyoua mifugo 25,000

UKURASA 2

## Soko lingine Dar lateketea kwa moto, laleta hasara

UKURASA 3

MICHEZO YANGA NA HESABU KALI KWA BIASHARA UK.24
MAONI, KATUNI UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan (katikati) akishuhudia Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Frank Nyabundege (kushoto) na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Maendeleo ya Ufaransa (AFD), Rioux Remy wakitia saini mkataba wa mkopo wa masharti nafuu wenye thamani ya Sh. bilioni 210 na msaada wa kiufundi wa Sh. bilioni 2.6 wenye lengo la kuimarisha TADB kufikia kutoa mikopo ya muda mfupi na mrefu katika sekta ya kilimo nchini. Hafla hiyo ilifanyika katika mji wa Brest nchini Ufaransa mwishoni mwa wiki. **PICHA: IKULU**

# Sakata Ngorongoro lawagawa wabunge

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

MVUTANO mkali umetokea kati ya pande mbili za wabunge wanaounga mkono hatua ya kupunguza watu ndani ya Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA) na wanaopinga uamuzi huo.

Aidha, wamemshauri Spika, Dk. Tulia Ackson, kuunda kamati teule kwenda kuchunguza jambo hilo.

Hayo yalijitokeza mwishoni mwa wiki wakati wa semina ya wabunge iliyoandaliwa na NCAA kwa maelekezo ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Mbunge wa Viti Maalum, Riziki Lulida, alisema aliwahi kuwa mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi na Maliasili, iliyokwenda a na kukuta zinajengwa hoteli karibu na eneo la creta waliagiza ujenzi usiendelee.

Alisema wanaojenga nyumba za kudumu ndani ya hifadhi siyo wafugaji pekee, bali hata watumishi wastaafu wa hifadhi hiyo, na kwamba kuna maswali mengi kuwa wanatoa wapi vibali na vinaidhinishwa na nani, na ilipendekezwa waondolewe, lakini waliendelea kuwapo humo hadi sasa.

Naye Mbunge wa Biharamulo Magharibi, Ezra Chiwelesa, alisema nchi ni kubwa watu wanaweza kupunguzwa na kupelekwa maeneo mengine, huku akihoji ukubwa wa kata zenye kijiji kimoja huku wakitumia zaidi ya Sh. bilioni 35 kupewa huduma zote muhimu.

"Wenzetu wa Ngorongoro kata moja ina kijiji kimoja, mimi nina kata yenye watu 27,000, wanapewa fedha kila mwaka, wanajengewa huduma zote muhimu za kijamii na bado watoto hawaendei shule wanafuga," alisema.

Naye Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Hawa Bananga, alisema walipoenda walijikuta kwenye mazingira magumu kwa kuwa wanafuatiliwa kila walipokwenda na wakiongea tofauti na matakwa ya wenyeji wanakuwa kwenye hali ngumu.

"Ifike mahali serikali ifanye uamuzi, hali ni mbaya sana unapoingia tu unakutana na mifugo inaharibu mazingira, wanafuga kondoo ambao wanakula hadi mizizi na kung'oa uoto wa asili," alisema.

"Leteni sheria bungeni tubadilishe, wapo waliotufuata wako tayari kuhama hata kesho, ila wanalazimishwa na wachache wanaonufaika kuendelea kukaa mle."

Naye Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, alisema kuna watu wachache wenye mifugo mle ndiyo wanashinikiza wengine kukataa kuondoka, ila baadhi wako tayari, hivyo ni bora ukaandaliwa utaratibu.

"Ukishazaa mtoto siyo mali yako bali ya Tanzania, kule tuna watoto hawasomi wanachunga mifugo tu, wanaonufaika watoto wao wanasoma shule nzuri na wanatibiwa Ulaya na Marekani," alisema.

Naye Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Kaita, alisema ni muhimu serikali ikaangalia sheria kwa kuwa haikusema idadi na hifadhi imepata sifa za kimataifa kwa kuwa na mchanganyiko wa binadamu na wanyama.

"Wanaozungumzia Ngorongoro wanaeleza upande mmoja wa wanyama, mifugo, watu na uharibifu wa mazingira hakuna aliyeeleza faida ya watu walioko mle. Mmeacha yamejengwa maghorofa na nyumba za bati nani katoa vibali?" Alihoji.

Naye Mbunge wa Viti Maalum, Asha Abdallah Juma, alisema ni muhimu serikali ikaharakisha kuleta Muswada wa Mabadiliko ya Sheria kwa kuwa hali ikiiachwa ilivyo urithi wa dunia utapotea.

Mbunge wa Korogwe, Timotheo Mzava, alisema Serengeti na Ngorongoro zinategemeana na unapoua mmoja lazima na mwingine afe, na kutaka hatua za haraka kuchukuliwa kuokoa maisha ya watu na maliasili.

Mbunge wa Simanjiro, Chrostopher Ole Sendeka, alisema "Hakuna anayekataa ongezeko la wananchi, lakini hakuna anayeeleza ongezeko la hoteli na camp ambazo zinachukua maji Creta."

"Namwomba Spika aunde kamati teule iende Ngorongoro, Bunge lisifanye uamuzi wa upande mmoja. Sina tatizo watu kuhamishwa, ila lazima haki za binadamu zizingatiwe na tuelezwe kwanini watumishi wastaafu wa NCAA waliendelea kubaki na kujenga nyumba za kisasa na hawajachukuliwa hatua," alisema.

Mbunge wa Ngorongoro, Emmanuel Oleshangai, alisema ni muhimu wafugaji wakasikilizwa na kwamba wanaosema mifugo inatoka nje siyo kweli, huku akieleza kuwa tembo waliokufa walikula maboga eneo la Karatu, na kwamba kesi za ujangili zilizopo mahakamani ni za watumishi wa NCAA na siyo wafugaji.

"Serikali isikilize wananchi na siyo kupeleka vifaru, lazima tujadiliane. Kuna hoteli ndani ya creta inatuchukulia maji kwenye creta, tunataka mkiondoa watu na hizi hoteli mziondoe," alisema.

Mbunge wa Ubungo, Prof. Kitila Mkumbo, alisema mkataba wa UNESCO unataka kulinda binadamu na inapotokea mgogoro atalindwa binadamu, na pia ilani ya CCM inasema ikitokea mgogoro kati ya wanyama na binadamu haki ya binadamu italindwa.

"Hapa kuna mambo matatu tu yakufanyika ambayo ni kutumia mabavu kuwaondoa, kuwalipa fidia waondoke na kuwahamasisha waondoke kwa hiari. Kwanini serikali inashindwa kutumia mbinu hizi?"

Mbunge wa Viti Maalum, Ester Matiko, alisema inashangaza kuwa Baraza la Wafugaji lina nguvu kuliko serikali licha ya kuwa chini ya waziri na linapewa fedha na kuzitumia litakavyo huku walengwa hawanufaiki.

Mbunge wa Viti Maalum, Cecilia Pareso, alisema Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ilieleza namna mimea vamizi inamaliza malisho ya wanyama na mazalia ya nyumbu yalivyoharibiwa.

"NCAA inasomesha watoto hadi vyuo vikuu, mbona wa maeneo mengine hawasomeshwi, kila mara Manyara tunapokea wamama na watoto kutoka hifadhini wanakuja kuomba chakula kwasababu hali mbaya, fedha zinazotolewa zinamnufaisha nani?" Alihoji.

Mbunge wa Rorya, Hassan Chenya, alisema wananchi hao wanakosa haki za huduma za jamii zinazotolewa na serikali kwa sababu hawana pa kuzijenga na mara kadhaa wamepelekewa fedha, na kwamba ni aibu mbunge kuendelea kuongoza watu maskini, wasio na huduma za afya na mazingira magumu ya maisha.

# Mifugo 25,000 yafa kwa ukame

**Na Allan Isack,** KITETO

MIFUGO zaidi ya 25,000 ya wafugaji wa Wilaya ya Kiteto mkoani Manyara ikiwamo ng'ombe imekufa kwa kukosa maji na malisho kutokana na ukame ulioikumba wilaya hiyo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Kiteto, Mbaraka Batenga, kufa kwa mifugo hiyo kumeacha maafa makubwa kwa kaya, hasa zinazotegemea shughuli za ufugaji kuendesha maisha yao.

Batenga alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya kupokea lambo kubwa la kisasa, lililojengwa kwa ufadhili wa Kampuni ya Sunset, katika Kijiji cha Katikati.

"Wilaya yetu imepoteza mifugo mingi kwa kuwa ilikosa maji na majani ya malisho kutokana na ukame uliokithiri,"alisema Batenga.

Vilevile, alisema kutokana na adhaa ya maji katika eneo hilo, wanyamapori wamekuwa wakivamia vijiji kutafuta maji huku wengine wamekuwa wakitumbukia katika visima vya asili vilivyochimbwa na wananchi.

Pia alisema kutokana na ukame kukithiri wanyamapori wamekuwa wakiingia katika mashamba ya wakulima na kuharibu mazao yaliyokuwa shambani.

Batenga alisema: "Kijiografia wilaya yetu ni kame, mvua hazinyeshi kwa kipindi chote cha mwaka, japokuwa ni wazalishaji wazuri wa mazao ya chakula na biashara. Hata hivyo, tumekuwa tukitumia vizuri mvua chache zinaponyesha."

Baada ya makabidhiano hayo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Katikati, Nongoyoo Lengobe, alisema lambo hilo, litasaidia kutatua adha hiyo kwa wananchi, mifugo na wanyamapori, kwa kuwa watapata sehemu ya kwenda kunywa maji.

"Kabla ya kuchimbwa kwa lambo la mifugo na wanyamapori, mifugo ilikuwa ikiteseka na mingine ilikuwa ikitumbukia visimani," alisema Lengobe.

Aidha, alisema kujengwa kwa lambo hilo wananchi zaidi ya 13,000 wa kijiji hicho watapata huduma ya maji nyakati za ukame.

Mwekezaji wa Kitalu cha Uwindaji cha Makame-WMA, ambaye ni Mkurugenzi wa Kampuni ya Sunset, Saleh Alamry, alisema wametumia zaidi ya Sh. milioni 600 kutekeleza mradi wa kuchimba lambo hilo.

Alisema kampuni hiyo ilifikia hatua kusaidia uchimbaji wa mradi huo kwa kuwa wananchi wa eneo hilo walikuwa wanakabiliwa na tatizo la maji.

Kadhalika, alisema maji ya visima yaliyokuwa yanatumiwa na wananchi yalikuwa na kiwango kikubwa cha chumvi na hayafai kwa matumizi ya binadamu.

"Maji yakikauka wakati wa kiangazi wanawake wanachimba kwenye matope kwa ajili ya kutafuta maji na endapo ikitokea wananunua dumu wanauziwa Sh. 200 hivyo kampuni iliguswa kujitolea kuwasaidia.

Alisema upana wa lambo hilo ni mita 300 urefu ni wa kilomita moja na urefu wa kwenda chini ya ardhi ni mita 10.

## HABARI KITAIFA

### KESI YA MBOWE

# Shahidi aliyeugua ghafla kizimbani kuendelea leo

Na Kulwa Mzee

SHAHIDI wa 13 wa upande wa mashtaka katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu, Inspekta Tumaini Swila anatarajia kuendelea kutoa ushahidi leo.

Shahidi huyo aliugua ghafla akiwa kizimbani mwishoni mwa wiki, baada ya kuulizwa maswali na wakili wa upande wa utetezi, Peter Kibatala.

Inspekta Swila ataendelea kutoa ushahidi wake Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga.

Shahidi huyo alianza kutoa ushahidi Februari 2, mwaka huu kwa kuongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando hadi Februari 9 alipoumwa ghafla wakati akihojiwa na wakili wa utetezi, Peter Kibatala.

Februari 9, mwaka huu, kesi iliahirishwa hadi Februari 10, kwamba shahidi alitakiwa kufika mahakamani kuendelea na ushahidi lakini hakutokea kwa madai alishauriwa na daktari apumzike.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Nassoro Katuga, alidai shahidi hakuweza kufika mahakamani kuendelea na ushahidi, alishauriwa na daktari apumzike, hivyo hawataweza kuendelea kinyume na ushauri wa daktari.

Wakili Katuga aliomba kuahirisha kesi hadi leo kama shahidi atakuwa hajapona wanaweza kutafuta shahidi mwingine.

Jaji Tiganga alisema mahakama ina nia ya kumaliza shauri hilo kwa haraka, mahakama iliahirisha shauri hilo hadi leo.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani ambao wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei Mosi na Agosti 5, mwaka 2020.


ENEO LA BIASHARA LINAPANGISHWA KWA MUDA MREFU [MIAKA 15-20] AU KUUZWA.

ENEO LA BIASHARA LENYE UKUBWA ZAIDI YA SQUARE METER 5,800 AMBALO LIPO MAENEO YA BARABARA YA MANDELA KARIBU KABISA NA UWANJA WA TAIFA DAR ES SALAAM.

[Mwenye ofa kubwa atapewa kipaumbele]
MAWASILIANO
0762215470 MR MATHIAS
0682243694 MR. VALENCE


# Karume waomba mtaji kwa Rais Samia

Na Mary Geofrey

WAFANYABIASHARA katika Soko la Karume jijini Dar es Salaam, wamemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuwapatia mitaji ili kukuza biashara zao.

Wakizungumza na waandishi wa habari, mwenyejiti wa wafanyabiashara hao, Jumanne Kongogo, aliwasilisha kilio hicho wakati wakitoa shukrani kwa serikali baada ya kuunguliwa na mali zao na kuruhusiwa kujenga vibanda.

"Uamuzi wa Rais Samia tujenge maeneo yetu ya kufanyia biashara ulitupa amani sana wafanyabiashara. Kweli tumejenga mabanda yetu wenyewe lakini changamoto ni kukosekana kwa mitaji kwa wafanyabiashara," alisema.

Alieleza kuwa, mabanda yote yameshajengwa kwa uratatibu mzuri wa kuacha nafasi za kupitisha magari ili inapotokea dharura kuwa na njia ya kupita, lakini mabanda mengine hayana biashara kwa sababu watu hawana mtaji wa kuanza upya.

Aliomba serikali kuwashika mkono kwa kutoa kiasi chochote cha fedha kwa ajili ya kuwainua wafanyabiashara ambao wametengeneza mabanda, lakini hawana fedha za kununua mizigo ya kuuza.

"Wengi walipata taarifa soko limeungua pengine hawajafahamu bado kama soko limerejea ndiyo sababu bado wanasuasua kujitokeza kununua bidhaa hapa sokoni," alisema Kongogo.

Aidha, alisema wafanyabiashara 3,700 katika soko hilo, wamepata maeneo ya kufanyia biashara na wachache waliokosa bado wanaendelea kutafutiwa maeneo.

"Leo tumewaita waandishi wa habari ili kutoa shukrani zetu kwa Rais Samia kwa kutukubalia maombi yetu ya kurejea kwenye maeneo yetu ya biashara, kitendo hiki kiliwapa faraja sana kwa sababu walikuwa na huzuni mbili za kuunguliwa na biashara na kutoruhusiwa kuendelea kufanyabiashara," alisema Kongogo.

Alisema wafanyabiashara walihofia kuwa huwenda soko hilo lingesubiri kujengwa na serikali kwa muda mrefu na hivyo kuchelewesha biashara zao.

Naye mfanyabiashara wa batiki, kanga na vitenge katika soko hilo, Betty Mtewele, aliiomba serikali kuwasaidia kupata mitaji.

Mfanyabiashara mwingine, Hermina Kauka, alimshukuru Rais Samia kwa kutambua kundi la wafanyabiashara kama kundi maalum linalotambulika rasmi.

Alisema biashara zao zimekwama wanashindwa kutoa marejesho ya vikoba, wanachama nao wanashindwa kuendelea kuweka akiba kwa sababu wanatafuta kwa ajili ya kujikimu na kuongeza mitaji.

# Moto wateketeza tena mali Soko la Mbagala

Na Jenifer Gilla

IKIWA imepita takribani mwezi mmoja tangu kuungua moto kwa Soko la Karume jijini Dar es Salaam na kuteketeza vibanda na mali za wafanyabiashara, tukio hilo limewakuta pia wafanyabiashara wa Soko la Mbagala Rangitatu.

Usiku wa kuamkia jana, moto mkubwa uliwaka katika Soko la Mbagala Rangitatu wilayani Temeke, na kuteketeza mali za wafanyabiashara wa soko hilo.

Hadi kufikia jana mchana, bado moto huo ulikuwa unawaka kwenye baadhi ya maeneo ya soko hilo, huku Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kushirikiana na raia wakiendelea kuuzima.

Akizungumzia tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, alisema chanzo cha moto huo bado hakijajulikana lakini wameunda kamati itakayokuwa na jukumu la kufanya uchunguzi ili wafanyabiashara hao waendelee na biashara zao mapema.

"Tumeunda kamati kuchunguza chanzo cha moto huo na tumeipa siku tatu hadi nne, kikubwa tumetoa maelekezo kwa manispaa kamati ya uchunguzi ikikamilisha kazi wafanyabiashara waruhusiwe kurudi sokoni kufanyabiashara huku ikiwekwa mipango ya kukarabati na kuboresha soko hilo," alisema Jokate.

Jokate aliwaomba wafanyabiashara hao kuwa na subira katika kipindi hiki ambacho kamati hiyo imeundwa kwa ajili ya kuchunguza chanzo cha ajali hiyo na kujua hasara iliyopatikana.

"Tunaomba muwe na subira kamati itafanya kazi yake kwa siku tatu kufanya uchunguzi wake pamoja na taratibu zingine za kuboresha soko ili kuruhusu shughuli zingine kuendelea katika soka hili," alisema Jokate.

Alisema soko hilo lilikuwa na vizimba 388 na vibanda 20 ambavyo vimeungua, kwamba wanalishukuru Jeshi la Zimamoto na Uokoaji waliwahi mapema na kusaidia kuokoa na walifanikiwa kutokana na miundombinu ya soko kuwa mizuri ikiwamo barabara zinazopitika.

**MATUKIO YA MOTO**

Januari 16, mwaka huu Soko la Karume jijini Dar es Salaam liliteketea kwa moto na kusababisha hasara kwa wafanyabiashara, huku chanzo chake kikitajwa kuwa ni mshumaa uliowashwa na 'mateja'.

Kadhalika, Februari mosi mwaka huu moto uliteketeza sehemu ya Soko la Mbuyuni lililoko katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro na kusababisha hasara ya mali kwa wafanyabiashara wa soko hilo.

Vilevile, Julai 10, mwaka jana moto uliteketeza Soko la Kimataifa la Kariakoo, jijini Dar es Salaam na kusababisha hasara kubwa kwa wafanyabiashara.

Akizungumza viongozi wa machinga wa Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, Ikulu jijini Dar es Salaam Januari 25, 2022, Rais Samia Suluhu Hassan aliwataka wamachinga kujisimamia na kuepukana na masuala yanayohatarisha usalama wa masoko na kuhakikisha ujenzi wa vibanda vipya vya Soko la Karume unazingatia uwapo wa nafasi zitakazowezesha magari ya zimamoto kupita wakati majanga yanapotokea.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI

Anwani ya Simu: "Uvuvi"
Simu Nambari: +255 (026) 2322612
Nukushi: +255 (026) 2322613
Barua pepe: ps@uvuvi.go.tz
Tovuti: http://www.mifugouvuvi.go.tz

Mji wa Serikali Mtumba,
Mtaa wa Ulinzi,
S.L.P 2847,
40487 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

KUFUNGULIWA KWA MSIMU WA UVUVI WA KAMBAMITI KWA MSIMU WA MWAKA 2022 (TANGAZO LIMERUDIWA)

Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi) inapenda kuwatangazia wananchi wote kwa mara nyingine kwamba uvuvi wa Kambamiti (Prawns) kwa msimu wa mwaka 2022 utafunguliwa tarehe 1 Machi mpaka tarehe 30 Septemba, 2022 kwa Kanda ya Kaskazini (Dar Es Salaam, Tanga, Bagamoyo na Saadani) na tarehe 01 Aprili hadi tarehe 31 Agosti, 2022 kwa Kanda ya Kusini (Kisiju, Rufiji Delta, Jaja/Kilwa, Lindi na Mtwara).

Kutokana na rasilimali za Kambamiti zilizopo, Wizara husajili meli 12 kufanya uvuvi wa kambamiti kwa kila msimu wa uvuvi huo. Aidha, katika tangazo la awali lililotolewa katika magazeti tarehe 15 Novemba, 2021, jumla ya maombi kumi yalipokelewa na kufanyiwa uchambuzi ambapo ni meli tano (5) ndiyo zimekidhi vigezo vya kufanya uvuvi huo.

Kutokana na hali hiyo, Wizara inatoa tena muda wa siku saba (7) kuanzia tarehe 14 hadi 20 Februari 2022 kwa wananchi au Kampuni ambazo zina meli zenye sifa kuwasilisha ombi la kufanya uvuvi huo ili kukamilisha idadi ya meli 12 zinazotakiwa kwa m simu wa mwaka 2022. Aidha, wananchi na Kampuni zilizokosa sifa kwa maombi yaliyowasilishwa kwenye tangazo la awali, vinapewa fursa ya pili ya kuwasilisha maombi yao ikiwa vitakuwa vimekidhi vigezo vinavyotakiwa.

Waombaji wanapaswa kuzingatia Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003, Kanuni za Uvuvi za mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2020, Kanuni za TASAC za Usajili wa Meli za Kibiashara za mwaka 2005 pamoja na Miongozo na Taratibu nyingine za Nchi.

Aidha, vigezo vya kuzingatia katika maombi ya uvuvi wa Kambamiti vinapatikana katika Tovuti ya Wizara (**www.mifugouvuvi.go.tz**) na katika Ofisi za Wizara Kanda ya Dar Es Salaam na Pwani.

Imetolewa na:
DKt. Rashid A. Tamatamah
KATIBU MKUU-UVUVI

216703302

## MIAKA 2 YA MWL. ORONDE;

# Aitoa sekondari mkiani na uhalifu kibao, hadi kung'ara na nidhamu

**Na Salome Mwasamale**

## ●Mbondole; mtihani vinara daraja '0'
## ●Wanafunzi 'walioana'; vibaka porini
## ●Aliwasoma mwezi mzima, akawaelewa



Wanafunzi wa sasa wa Shule ya Sekondari Mbondole.

NI simulizi yenye ukakasi kusikia shule ambayo miaka mitatu iliyopita ilikuwa imetawaliwa na matokeo 'divisheni ziro' si chini wanafunzi 100 kila mwaka na katika nafasi ya tatu kutoka mwisho kimkoa.

Pia ni jambo lililombatana na utovu wa nidhamu kufikia kiwango cha uhalifu hatari ngazi ya kumshikia silaha mkuu wa shule kwa lugha 'nitakushikisha adabu'; wanafunzi kuporana baiskeli baadhi wanashinda porini wakijiunga na 'vibaka' kuvizia wapita njia na wenzao wanaoenda masomoni.

Leo hii ni miaka miwili tu kupita, hadithi ya shule hiyo inageuka ghafla upande wa pili sasa, ikivuta tabasamu ya wadau wake matokeo ya 'diviseni ziro' kwa waliofanya mtihani ni wanne tu kutoka miaka wastani wa 100 awali, nidhamu bora imetawala shuleni... ajabu na kweli!

Hapo ndipo inarejewa methali 'usione vinaelea vimeundwa' akitajwa Mkuu Mpya wa Shule ya Sekondari Mbondole iliyoko kata ya Msongola Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, umbali wa kilomita tatu kutoka barabara kuu ya lami kutoka Mbagala kwenda Chanika, Boniface Orenda, anayetwikwa ushujaa na kipenzi cha wazazi, majirani, hata uongozi wa kata.

Mwalimu Orenda anaisimulia Nipashe kwamba Sekondari ya Mbondole ilianzishwa Machi 15, 2007 huku asilimia 80 ya wanafunzi wakitokea Shule ya Msingi Mbondole, sehemu kubwa ya wazazi wao wanatoka katika jamii ya wafugaji wanaoishi jirani.

Anarejea hali mbaya ya kitaaluma iliyotokea ni kwamba mwaka 2016 Mbondole haikuweza kupata mwanafunzi aliyefaulu daraja la kwanza wala la pili na la tatu walikuwa watatu, daraja la nne 18 na daraja sifuri 102.

Pia anataja mwaka mmoja kabla ya kuja kwake mwaka 2019, shule haikupata daraja la kwanza, la pili na daraja la tatu, huku 10 pekee wakiwa wa daraja la nne 104 na wasioambulia kitu walikuwa 124.

**SIRI YA MAGEUZI**

Ni swali la Nipashe ambalo Mwalimu Orenda, alianzia na majibu yake kuhusu uteuzi wake kutoka Shule ya Sabodo Sekondari alikokuwa Makamu Mkuu wa Shule, akiwa na ufafanuzi:

"Taarifa hii niliipokea kwa mshtuko hasa kutokana na taarifa za matukio mbalimbali ya kihalifu yaliyokuwa yakifanywa na wanafunzi wa Mbondole ikiwamo matumizi ya silaha zenye ncha kali kama vile bisibisi, nyembe, visu, panga."

Pia anataja uhalisia wa ripoti zilizomfikia kuhusu shule hiyo ni namna ilikuwa taabani kwa ngazi ya taaluma kimkoa, ufaulu ikiburuza mkia, lakini akaamua kujikaza kuwajibika kwa kuripoti katika kituo kipya cha kazi.

Hapo akajipa mwezi mmoja kuyasoma mazingira kabla kuanza 'operesheni kurekebisha' tangu aliporipoti kazini Januari Mosi mwaka 2020, akieleza hatua ya kwanza ilikuwa kujifunza tabia ya wanafunzi ili kuthibitisha alichokisikia, kusoma tabia za watendaji wake, majirani wanaozunguka na ndipo akajiridhisha kwa ajili ya kuamua.

Anataja alianza kwa kufanya ubunifu ndani ya shule kurejesha nidhamu, ikiwamo unadhifu wa wanafunzi na kufuatwa taratibu zote zas shule, huku nje ya mipaka akiwafutilia wanafunzi wanaotajwa watukutu, wasiohudhuria masomo na wahusika wa uhalifu.

Baada ya kupata picha upana, Orenda anasema alianza kukabiliana na tatizo moja baada ya lingine, akianza na nidhamu kwa imani ndio penye suluhisho la vyote, ikiwamo matokeo mazuri shuleni, jambo analojivuna amefanikiwa kukabiliana kwa asilimia 100, hata kinachoongolewa leo kubaki historia.

Mkuu wa Shule anasimulia amelazimika kutumia ushirikiano wa mamlaka za kata, wakiwamo



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Mbondole, Boniface Orenda. **PICHA ZOTE: SALOME MWASAMALE**

mgambo kukabili wanafunzi, pia wakazi majirani kuwasaidia kupitia kamati za wazazi kila darasa akiweka viongozi wanane, yaani mwenyekiti, katibu na wajumbe sita.

**WENYEJI WANENA**

Mkuu wa Shule anaungwa mkono na simulizi ya mama mkazi jirani, Rachel Sibusi maarufu kama mama John, anayeeleza kwa uchungu shule hiyo imemuumiza sana kimaisha, watoto wake wanne wamepita wakipata alama sifuri, kati ya mwaka 2016 na 2020.

"Mwaka huu 2022 chini ya Mwalimu Orenda ninaye mtoto wangu wa mwisho John Peter ambaye anafanya mtihani naamini ataniletea japo cheti naanza kuyaona," anasema.

Pia, analalamia kuwapo tabia wakati huo wanafunzi wanaokaa porini mithili ya mke na mume wanapika vyakula na baadaye wanaingia darasani, hata wanapoulizwa hujibu "yako yalikushinda acha tufanye yetu, hayakuhusu..."

Pia Mama Rachel anatoa ushuhuda wa walimu wakatio huo kupigwa na wanafunzi waliowavizia njiani.

Wanafunzi Antony Chuhila na Naomi Fungo, walioko kidato cha tatu waliohojiwa na Nipashe wanakiri kushuhudia uhalifu uliokithiri shuleni kwao, hata mmoja akiwa na ushuhuda wa kunusurika kuporwa na wenzake baiskeli yake ya kuendea shule wakiwa kidato cha kwanza.

"Hali ilikuwa mbaya zaidi kwa kuwa tulikuwa tunazuiliwa njiani na wanafunzi wakubwa na kututishia kutupora wakati mwingine wanakupiga na kukuacha na majeraha, lakini sasa uhalifu huo hakuna tuna amani ya kutosha," anaeleza Antony.

Anasema kila timu ilihusika na kusimamia nidhamu, maendeleo ya taaluma pamoja na uboreshaji miundombinu ya kusoma, kwa kushirikiana na walimu. Pia, kukawapo kamati mama ya shule, chini ya Mwenyekiti anayemtaja Komredi Nassoro Ally Nassoro.

Orenda anataja pia kuhusisha viongozi wa dini zote aliowapa nafasi kuwahudumia watoto kiroho, akiamini utii kwa Muumba kungewafikisha mbali, huku nafasi nyingine wakipewa viongozi wa Serikali Mtaa wa Mbondole.

Hapo anamtaja Mwenyekiti, Thomas Nyanduli na mgambo wake waliomsaidia kuingia porini na kuwakamata wanafunzi waliokuwa wakitumia silaha na kujificha huko, hata wakawafikisha katika vyombo vya sheria.

Pia anataja hatua ya kuwahamasisha wazazi na wananchi wa jirani kuitumia fursa ya shúle hiyo na mazingira yake, kuwa mkombozi wa watoto wao familia zao, ambao anasema walimuwelewa kwa kutoa taarifa nyingi za uhalifu na kufanikisha kuwakamata na kisha kuwafikisha polisi.

**ALIVYOONJA 'JOTO YA JIWE'**

Wakati akiwa katika mpango mkakati akiwa mgeni kukabili mazito ya kituo chake kipya, ikiwamo kupambana na 'wanafunzi wahalifu' kumbe nao walijipanga kumkabili 'adui' mkuu huyo mpya wa shule.

Wanafunzi hao wengi wahitimu wa kidato cha nne mwaka 2020, anawataja walikuwa watukutu mno hata kufikia hatua kumvamia ofisini na silaha hata akatumia mbinu za medani zikamwokoa ilhali kaonja makali ya wanafunzi wake, aliokuwa na simulizi zao.

**● Ilikuwaje mkasa wake ofisini 'hatua kwa hatua' na maisha mapya shuleni? Endelea kesho.**

# Mkopo wa bil. 60/- kunufaisha wajasiriamali Z'bar bila riba

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Benki ya CRDB, wamezindua mpango wa kuwawezesha wajasiriamali 700,000 kwa kuwapatia mkopo wa Sh. bilioni 60 kusaidia kuendeleza uchumi wa buluu visiwa humo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akizindua mpango huo mwishoni mwa wiki wa 'Inuka na Uchumi wa Buluu' katika hafla iliyofanyika Kikwajuni visiwani humo, aliishukuru Benki ya CRDB, akisema mikopo hiyo itachochea ukuaji wa uchumi.

Alibainisha kuwa uwezeshaji huo wa kifedha, utakwenda sambamba na mafunzo ya ujasiriamali kwenye mikoa yote visiwani humo, na kwamba wajasiriamali wa Unguja na Pemba wachangamkie fursa hiyo ya kipekee ili kukuza mitaji na kuboresha biashara zao.

"Juhudi zinazofanywa na Benki ya CRDB katika kujenga uchumi wa Zanzibar ni nyingi na ninaamini kwamba sasa zinafahamika vizuri. Serikali itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika katika kudumisha uhusiano mwema ulioko kwa faida ya pande zote mbili, pamoja na wananchi wote.

"Mmedhihirisha uzalendo wa kweli kwa kuandika historia ya kuwa benki ya kwanza nchini, kutoa mikopo bila riba kwa wajasiriamali. Hii inaonyesha dhamira ya kweli mliyonayo katika kuboresha maisha ya wajasiriamali hapa Zanzibar," alisema Rais Mwinyi.

Rais Mwinyi alisema wajasiriamali wote wazingatie taratibu za mikopo, huku akisema mikakati ya serikali ya kuwawezesha wajasiriamali, ni pamoja na utoaji wa vitambulisho, ujenzi wa masoko, utoaji wa mikopo yenye masharti nafuu, elimu, zana, mitaji pamoja na utaratibu mzuri wa kulipa kodi.

"Serikali itaendelea na juhudi za kuwapatia mitaji, masoko, elimu pamoja na kuweka mazingira rafiki ili waweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi," alieleza Rais Mwinyi.

Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Abdulmajid Nsekela, alisema kundi la wajasiriamali ni kundi la kimkakati katika maendeleo ya taifa kutokana na kujumuisha asilimia kubwa ya wananchi na pia zaidi ya ajira 100,000 zinatarajiwa kuzalishwa.

"Mheshimwa Rais utaratibu wa mikopo hii ni rahisi sana na tutakuwa tukiitoa kwa kushirikiana na serikali katika hatua zote za utambuzi na upitishwaji wa mikopo, ili kuhakikisha makundi yote stahiki ya wajasiriamali yananufaika," alisema Nsekela.

Alielezea utaratibu wa utoaji mikopo hiyo, kwamba utazingatia mazingira ya soko la Zanzibar na mikopo itatolewa kupitia mfumo wa kutoa huduma unaozingatia misingi ya dini ya kiislamu 'CRDB Al Barakah Banking', pamoja na mfumo wa kawaida kwa wahitaji.

"Shughuli zilizopewa kipaumbele katika mpango huu, ni zile ambazo zimeainishwa katika sera ya uchumi wa buluu ikiwamo uvuvi, ufugaji wa samaki na kilimo cha mwani.



Mkuu wa Wilaya ya Ilemela, Hassan Masala, akimkabidhi cheti kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, mmoja wa maaskari waliofanya vizuri kupambana na matukio mbalimbali ya kihalifu, katika hafla ya pongezi iliyoandaliwa na RPC wa Mkoa wa Mwanza, Ramadhan Ng'anzi. (kushoto). **PICHA: ROSE JACOB**

# 'Crain' yatumbukia Ziwa Victoria, dereva afa

**Na Richard Makore,** MWANZA

MASHINE ya kunyanyua vitu vizito (Crain), yenye uzito wa tani 50 imezama Ziwa Victoria ikiwa na dereva wake katika Daraja la muda la JPM lililoko eneo la Kigongo -Busisi wilayani Misungwi mkoani Mwanza.

Tukio hilo lilitokea saa 8 usiku wa kuamkia jana katika daraja hilo lililojengwa katika eneo hilo ili kupitisha vifaa kwa ajili ya ujenzi wa daraja la kudumu la JPM.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Mwanza, Ambwene Mwakibete, alithibitisha kutokea ajali hiyo, na kuwa mashine hiyo ilitumbukia ziwani baada ya kupita pembeni, hivyo kutumbukia ikiwa na dereva wake.

Alimtaja dereva aliyefariki kuwa ni Abass Twalib (30), ambaye alikuwa ni mfanyakazi wa kampuni ya China inayojenga daraja hilo.

Kamanda Mwakibete alifafanua kwamba, wakati kazi ya ujenzi ikiendelea usiku wa manane, dereva alikosea njia na kupita katika ukingo wa daraja la muda na hivyo mashine hiyo kumshinda na kutumbukia ziwani.

Aliongeza kuwa baada ya kupata taarifa za kuzama mashine hiyo ikiwa na dereva walianza kumtafuta ndani ya maji na kufanikiwa kumpata kesho yake asubuhi akiwa amekufa. Alisema mwili wa marehemu baada ya kuopolewa ndani ya maji, ulikabidhiwa kwa ndugu zake kwa ajili ya maziko.

Kuhusu mashine hiyo, alisema kuanzia kesho wataalamu wataanza kazi ya kuitoa ndani ya maji.

"Leo (jana) tumeaicha humo ndani ya maji, kwa kuwa ipo chini na tutaanza kazi ya kuitoa humo kuanzia wiki ijayo (kesho) kwa kushirikiana na idara zingine.

Kamanda Mwakibete alisema kazi hiyo ya ujenzi inafanyika usiku na mchana na kwamba mafundi na wafanyakazi wengine wanatakiwa kuchukua tahadhari za kiusalama katika kipindi chote wanapokuwa kazini.

# Mbaroni madai kuua mtumishi wa kanisa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi Mkoa wa Njombe linamshikilia, Daniel Mwilango (42) kwa tuhuma za kumuua kwa kumkata mapanga, Nickson Myamba (48), aliyekuwa Katibu wa Baraza la Walei la Kanisa Katoliki Parokia ya Makambako.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamisi Issah, alisema tukio hilo lilitokea Februari, 7 mwaka huu, majira ya usiku, kwamba Nickson Myamba aliitwa na mtuhumiwa kwa ajili ya makabidhiano ya ofisi.

Alisema mtuhumiwa alikamatwa eneo la Doma Wilaya ya Mvomero mkoani Morogoro akiwa njiani kuelekea Mkoa wa Njombe.

Kamanda Issah alisema mtuhumiwa huyo amekamatwa akiwa na vitu mbalimbali vya marehemu ikiwamo simu ya mkononi.

"Katika hali isiyo ya kawaida simu tuliyomkuta nayo mtuhumiwa ni simu ya marehemu alikuwa bado anayo yeye, kitu kingine alichokutwa nacho cha marehemu ni funguo mbalimbali ikiwamo na ile chumba ambacho tukio lilitokea," alisema Kamanda Issah.

Kamanda Issah alisema mtuhumiwa huyo amekiri na kuonyesha vitu mbalimbali alivyotumia katika mauaji hayo ikiwamo panga alilokuwa amelitupa katika choo, chuma alichotumia kumpiga marehemu, ndoo na vitambaa vilivyotumika kwa ajili ya usafi wa damu kwenye chumba yalipotendekea mauaji.

Kamanda Issa alisema mtuhumiwa alijiandaa na kutumia chuma kizito kumpiga mwenzake eneo la kisogoni.

"Alipopoteza fahamu alimwongezea tena chuma kingine pigo la pili na hili pigo la pili lilimsababishia huyu Nickson kufariki, alichokifanya huyu Daniel alitumia panga kuutenganisha mwili, alitenganisha kiwiliwili, kichwa na kifua kilikuwa sehemu yake halafu na kiuno na miguu kilikuwa sehemu yake," alisema Kamanda Issah.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Presha hizi sasa zitazidi kuwapoteza waamuzi

**LIGI** Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea tena mwishoni mwa wiki hii kwa kupigwa mechi nne na kisha wiki ijayo Jumatatu na Jumanne kuchezwa mechi nyingine za raundi ya 15.

Jumatano ya Februari 23, Mtibwa Sugar itakuwa mwenyeji wa vinara wa ligi hiyo, Yanga katika mchezo wa kuhitimisha mzunguko wa kwanza msimu wa 2021/22. Yanga ambayo ipo kileleni ikiwa na pointi 36, tano zaidi ya watani wao wa jadi, Simba ndiyo timu pekee ambayo haijapoteza mechi hata mmoja msimu huu.

Hata hivyo, licha ya Yanga kuongoza ligi, imeongeza presha kubwa kwa waamuzi baada ya Simba kushinda mechi yake ya raundi ya 15 dhidi ya Mbeya Kwanza na kupunguza wigo wa pointi kuwa tano, lakini vinara hao wa Ligi Kuu wakiwa na mechi moja mkononi.

Kwa ujumla suala la waamuzi kushindwa kutafsiri vema sheria 17 za soka na kufanya makosa ama kwa kutokujua, kwa makusudi, makosa ya kibinadamu, mapenzi binafsi kwa timu moja au pengine kwa kurubuniwa limekuwa si jambo geni katika ligi hiyo.

Lakini si Simba, Yanga ama Azam pekee ambazo hazijawahi kunufaika na makosa ya waamuzi au kubinywa pale ambapo visivyo halali na mwamuzi kuamua vinginevyo. Lakini hofu inaonekana kuwa kubwa sana kuanzia kwa mashabiki wa Yanga, viongozi wa klabu hata wale wa serikali wenye mapenzi na klabu hiyo.

Hivi karibuni tulishuhudia Waziri wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba ambaye ni mpenzi mkubwa wa Yanga, akitoa malalamiko yake kwa waamuzi kupitia mtandao wake wa kijamii wa Instagram huku akiweka video fupi ya mshambuliaji wao, Fiston Mayele akinyimwa nafasi ya kufunga kwa madai ya kuotea.

Waziri Mchemba aliendа mbali na kueleza kwamba atapendekeza bungeni serikali inunue mitambo ya Teknolojia Maalum ya Kumsaidia Refa uwanjani (VAR), ili kuondoa makosa kama hayo.

Fukuto hilo liliendelea kushika kasi kwa viongozi wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Yanga, Hassan Bumbuli na Haji Manara kujitokeza mbele ya wanahabari wakilalamika kuwa Simba inabebwa kwa kupewa penalti nyingi, wachezaji wa timu pinzani kuonyeshwa kadi nyingi nyekundu, lakini katika mechi zao ikipewa muda mwingi wa nyongeza.

Haikuishia hapo wazee wa klabu hiyo waliibuka na kilio kama hicho huku wakieleza wataandamana kwenda Ikulu kutoa kilio chao cha Yanga kubinywa na waamuzi kwa Rais Samia Hassan Suluhu.

Kama hiyo halitoshi, presha hiyo kwa waamuzi ikaendea bungeni kwa wabunge mbalimbali sasa kufika mbali hadi kulitupia lawama Shirikisho la Soka nchini (TFF), kuwa linahusika na waamuzi kuboronga, jambo ambalo Nipashe tunalipinga kwa nguvu zote hasa tukizingatia namna ambavyo TFF imekuwa ikiwaadhibu.

Aidha, Nipashe pia tunawataka mashabiki, viongozi wa klabu na wadau wote wa soka kupunguza presha kubwa ambayo imekuwa ikielekezwa kwa waamuzi, kwani kwa kufanya hivyo kutawasababishia kuchezesha kwa hofu hususan zinazoihusu Simba.

Kwa mantiki hiyo, Nipashe tunawasisitiza waamuzi kuzingatia zaidi sheria 17 za soka hata kama patatokea mechi moja penalti nne ama kadi nyekundu tatu au zaidi endapo zinastahili zitolewe na si kushindwa kufanya hivyo kwa sababu tu ya malalamiko yanayoelekezwa kwao.

Tunataka kuona mchezo wa kiungwana 'Fair Play' katika mechi zote za Ligi Kuu Bara na si waamuzi kujawa na hofu kutokana na presha kubwa zinazoelekezwa kwao na baadhi ya klabu, hivyo kushindwa kuzingatia sheria 17 za soka.

Tunatambua wazi nguvu kubwa zilizonazo za kushawishi klabu hizi kongwe mbili; Simba na Yanga, hivyo tunachotaka kuona si klabu kupata matokeo kutokana na ukubwa wao, bali zote 16 zinazoshiriki ligi hiyo zitendewe haki katika mechi zao ili mwisho wa msimu tupate bingwa aliyestahili atakayeiwakilisha vema Tanzania katika michuano ya kimataifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuendesha klabu kwa hasara Mo Dewji hajapepesa macho

Na Adam Fungamwango

**WALA** si mtu wa kwanza kusema anaendesha klabu kwa hasara, bali wapo viongozi wengi huko nyuma wameshawahi kuongea jambo hilo.

Namzungumzia Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Mohamed "Mo" Dewji ambaye wakati wa maandalizi ya mechi ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika, pamoja mambo mengine alisema bado anaiendesha klabu hiyo kwa hasara.

Sitaki kuzungumzia mambo mengi aliyoongea, kuhusu kiasi cha pesa alizowekeza na kutoa kwa ajili ya mishahara, usajili, na kuendesha klabu hiyo, badala yake naunganisha maneno yake kwa ujumla kuwa kuendesha klabu hiyo bado kunampa hasara. Pamoja na mambo mengine mazuri aliyoongea, lakini baadhi ya wachambuzi na mijadala yao ikajikita hapo hapo kwenye kuiendesha klabu kwa hasara.

Baadhi walionekana kuwa na wasiwasi kwamba Simba inaendeshwa kwa hasara kwa madai kuwa yeye mwenyewe ana matangazo yake mengi kwenye klabu hiyo, akiweka mabango uwanjani na kwenye jezi.

Wapo baadhi ya watu wakiwamo wachambuzi wanaoamini kuwa klabu hiyo huenda inajiendesha kwa faida, lakini Mo hataki kusema ukweli.

Hata hivyo, kwa uchunguzi wangu mfupi nilichogundua ni kwamba mara nyingi anachoongea Mo, ndicho hujadiliwa zaidi, tena kwa asilimia kubwa ni hasi badala ya chanya.

Hilo hilo aliloongea Mo kwamba bado anaiendesha Simba kwa hasara, lakini wanajitahidi kuifanya baadaye iweze kujiendesha yenyewe, limeshawahi kuzungumzwa na Mkurugenzi wa Uwekezaji wa GSM ndani ya Klabu ya Yanga, ambaye ni Mjumbe wa Kamati ya Mashindano ya klabu hiyo, Injinia Hersi Said.

Novemba mwaka jana, akihojiwa na chombo kimoja cha habari kwenye mahojiano maalum, naye alisema kuwa klabu hiyo ya Yanga inajiendesha kwa hasara.

"Timu hizi zinajiendesha kwa hasara kwa miaka mingi, ndiyo maana zimekwama. Ukisema hivi mtu anaweza asikuelewe, lakini ukitazama mapato ya klabu na matumizi ndiyo utajua kwa nini zinajiendesha kwa hasara," alisema Injinia Hersi bila kupepesa macho.

Cha ajabu sikuona mtu au wachambuzi kuweka mijadala ya kumpinga au kuwa na wasiwasi kwamba ni kweli Yanga inaendeshwa kwa hasara au la. Ukweli lazima usemwe, kuwa kuanzia klabu ya Simba, Yanga, Azam na zingine zote nchini, sidhani kama kuna timu hata moja inajiendesha kwa faida.

Mashabiki wengi hudhani kuwa wingi wa wafuasi wa Simba na Yanga ndiyo unaoweza kusababisha klabu hizo kujiendesha kwa faida.

Ni kweli Simba na Yanga zina mashabiki wengi, lakini bado hakuna mifumo sahihi na ya moja kwa moja ya kuwatumia ili kupata pesa za kuziendesha klabu hizi kwa sasa.

Bado klabu hizi hazijamaliza kwa asilimia mia moja uwekezaji, hivyo bado wafanyabiashara na wawekezaji hawa wanatoa pesa zao mfukoni.

Kuna wanaojiuliza, mbona wanatoa tu pesa, wanafaidika na nini, au wanapata faida lakini hawasemi? Ukweli ni kwamba hawa waliowekeza ni wafanyabiashara wakubwa, ambao kwao kuwekeza pesa hata kwa miaka mitano siyo shida kwao, ili mradi wanajua kuwa hata baada ya miaka 10 wanaweza kuanza kupata faida. Siyo wachuuzi ambao wanauza bidhaa leo, jioni wanahesabu faida.

Kama wanaweza kujenga viwanda kwa muda mrefu na vikakamilika, wakavisajili, wakaanza kuajiri watu na kuanza uzalishaji ambao hawana uhakika faida itapatikana baada ya muda gani, lakini wanajua baadaye itapatikana, iweje kwenye soka wasifanye hivyo. Huu ndiyo unaitwa uwekezaji. Unawekeza sehemu ambayo unajua utatoa pesa kwa muda mrefu, lakini mwisho wa siku isiyo na jina itaanza kulipa.

Mo na GSM wanaweka matangazo yao kwenye jezi ni kwa ajili ya kupunguza makali ya kile wanachokiweka hapo na wala hayawapi faida kama zile wanazotoa kwenye usajili wa wachezaji, mishahara, kuwaweka wachezaji kambi, kuwasafirisha na gharama zinginezo.

Tuliona timu hizi pamoja na kuwa na wafuasi wengi huko nyuma, lakini hawakuweza kuzifanya kuwa tishio, badala ya kuishia kuwa ombaomba tu.

Labda kuwe na ajenda nyingine dhidi ya Mo, lakini kama ni kuziendesha klabu hizi, ukweli hata kwa macho unaona kuwa klabu za Tanzania bado zinaendeshwa kwa hasara.

## TANGAZO

# NAMNA YA KUTAMBUA STEMPU HALALI ZA KODI ZA KIELEKTRONIK (ETS)

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015




Stempu ya kodi ya kielektroniki **(ETS)** ni alama maalum **(label)** inayobandikwa au kuchapishwa katika bidhaa ili kuonesha kuwa bidhaa hiyo imelipa kodi.

Kwa kutumia **App** iitwayo **“Hakiki Stempu”** ambayo inapatikana kwa wenye simu janja (smart phones) aina zote mtumiaji wa bidhaa anaweza kuhakiki.




**HATUA ZA KUFUATA**

**1.** Pakua (download) App yako ya **“HAKIKI STEMPU”** kwa watumiaji wa **Android** kutoka **(Google Play)** na kwa watumiaji wa **iOS** kutoka **(Apple Store)** kwa kuandika neno **“HAKIKI STEMPU”** na kuinstall katika simu yako, kisha ukishakamilisha utaiona App husika katika simu yako.



**2.** Baada ya kuipakua na kuinstall, moja kwa moja fungua App hiyo na kisha ukurasa wa mwanzo (Splash Screen) utatokea ambapo Vigezo na Masharti **(Terms & Conditions)** zitaonekana ambapo utatakiwa kuzikubali **(Accept)** ili kuweza kuendelea mbele zaidi.




**3.** Kisha, App ya **“Hakiki Stempu”** itapenda kupata ruhusa ya kutumia kamera ya simu yako ili iweze kuscan bidhaa husika, hivyo utapaswa kukubali kwa kubonyeza kitufe cha **“OK”** na hapo App itakupeleka katika ukurasa wa **KuScan** bidhaa hiyo, ndipo utaweza kuhakiki alama za usalama kwa kuscan stamp yako iliyobandikwa kwenye bidhaa husika.



**4.** Eneo linalotakiwa kuwa scanned ni eneo **namba 2** kwenye **QR Code** kama inavyoonekana katika picha hapa.




**5.** Mara baada ya kulengesha kibox cha kuscan katika QR Code iliyo kwenye stempu, App itascan yenyewe na kukuuliza iwapo unaona mabadiliko ya rangi katika stempu iwapo ukiiangalia kwenye mwanga, na utabonyeza sehemu ya **“YES”** kama inavyoonekana katika picha.



**6. Hakiki Stempu** itakupatia majibu ya uhalali wa stempu iliyobandikwa katika bidhaa kama ifuatavyo,

**>>** Iwapo Bidhaa ni halali, basi simu yako itaonesha **namba** na **herufi** kama zilivyo kwenye stempu yaani; **jina la bidhaa, aina ya bidhaa, imezalishwa lini, jina la mzalishaji** na **namba ya Barcode.**



# 47 waliwa na wanyama, 165 kujeruhiwa miaka 6

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

WATU 47 wameuawa na wanyama wakali ndani ya Mamlaka ya Hifadhi Eneo la Ngorongoro (NCAA), kwa kipindi cha mwaka 2015 hadi Septemba 2021.

Aidha, watu 165 wamejeruhiwa vibaya ndani ya mamlaka hiyo na wanyama kama fisi, chui, nyati na simba kwa kipindi hicho.

Hayo yalielezwa mwishoni mwa wiki na Mtafiti Mwandamizi - Afya ya Mifumo ya Ikolojia Mstaafu wa Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI), Dk. Robert Fyumagura, wakati akiwasiliha mada ya hali halisi ndani ya Ngorongoro kwenye semina ya wabunge iliyoitishwa kwa maelekezo ya Waziri Mkuu.

Pia alisema tukio la karibuni ni la watoto watatu walioliwa na simba na mmoja kujeruhiwa vibaya.

Alisema ndani ya kipindi hicho pia ng'ombe 99, kondoo 444, mbuzi 250, punda tisa ambao jumla ni 842 waliliwa na wanyama mbalimbali.

Alisema, idadi ya mifugo ndani ya hifadhi hadi mwaka jana ilikuwa ni 1,074,000 ambao ni ng'ombe, mbuzi na kondoo, huku idadi ya watu ikiwa ni 110,000.

Aliongeza kuwa wakati hifadhi hiyo inaanzishwa mwaka 1959 watu walikuwa 8,000 na mifugo 261,889 huku takwimu za mwaka 2017 zikionyesha walikuwa watu 93,136 na mifugo 831,563.

"Changamoto za wenyeji wa eneo hilo ni asilimia 50 ni maskini, asilimia 64 hawajui kusoma na kuandika, asilimia tatu pekee ndiyo wanamiliki mifugo, mwaka 2021 uhaba wa chakula kwa wenyeji ulikuwa asilimia 75," alifanunua.

Dk. Fyumagura alisema nyingine ni ukame unaosababisha uhaba wa maji na malisho hasa uwanda wa chini, kuharibika kwa nyanda za malisho na kuenea kwa mimea vamizi aina 143 na kupungua kwa faru weusi kutoka 108 mwaka 1960 hadi 78 mwaka 2021.






# Wanaodaiwa kuwa wahamiaji haramu wakamatiwa mlimani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma linawashikilia watuhumiwa 53 wakiwamo wanaodaiwa kuwa wahamiaji haramu 45 kutoka Ethiopia wakiwa wamejificha katika Mlima Kolo Wilaya ya Kondoa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alisema wahamiaji hao walikamatwa Februari 11, mwaka huu, saa tatu asubuhi kwenye mlima huo wakiwa wamejificha.

Alisema wahamiaji hao walikuwa na umri kati ya miaka 15 hadi 25 na nia yao kubwa ni kusafiri kupita kwenda ughaibuni kinyume cha sheria.

Kamanda huyo alisema wahamiaji hao watafikishwa mahakamani.

Kwa upande wake, Ofisa Uhamiaji wa Mkoa Kamishna Msaidizi wa Uhamiaji Bahati Mwaifuge, alisema wahamiaji haramu 145 kutoka nchi za Ethiopia, Somalia na Pakistani wanashikiliwa mkoani Dodoma kutokana na kuingia nchini kinyume cha sheria.

Alisema wahamiaji haramu kutoka Ethiopia ni 132, Somalia tisa na Pakistani wanne.

## HABARI KITAIFA

## TMDA yatoa msaada wa mil. 7/-

**Na Salome Mwasamale**

MAMLAKA ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), imekabidhi msaada wa taulo za kike wenye thamani ya Sh. milioni 7 kwa taasisi ya watu wenye ulemavu ya Disabilities Community Development Organisation (DCDO) ili kufanikisha mradi wao wa hedhi salama kwa watoto wenye ulemavu.

Akikabidhi msaada huo Meneja Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa (TMDA), Gaudensia Simwanza, aliwataka viongozi na wanachama wa taasisi hiyo kuhakikisha mradi huo unatumika kwa lengo lililokusudiwa na kuwafikia watoto hao kwa wakati. "Tunaomba mjitahidi msaada huu uwafikie walengwa kama vile mlivyokusudia kwa kuwa tumeshuhudia baadhi ya taasisi zikipokea misaada na badala yake kutumia kwa ambalo halikukusudiwa, hivyo naomba ninyi msiige mfano huo," alisema.

Aidha, aliwapongeza kwa uamuzi wa kulisaidia kundi maalum la watu wenye ulemavu kwa kuwa linahitaji msaada huo kutokana na hali zao za kiuchumi kuwa duni.

Alisema TMDA ipo tayari kuendelea kushirikiana na (DCDO) katika kuhakikisha mradi huo na miradi mingine itakayoandaliwa inafanya vizuri na kuigusa jamii moja kwa moja.

Naye katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Kinondoni, James Mgego, aliyataka mashirika na jamii kwa ujumla kujitokeza kuunga mkono jitihada zinazofanywa na (DCDO) za kuwasaidia watu wenye ulemavu kwa kuwa ni kweli wanahitaji msaada kutoka kwa jamii.



Meneja wa Benki ya Absa Iringa, Sheilla Kajuna, pamoja baadhi ya wateja na wafanyakazi wenzake wakikata keki kusherehekea miaka miwili tangu benki hiyo ilipobadilisha jina kutoka Barclays na kuwa Absa. mjini Iringa mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madiwani wataka uwiano wa walimu shule za msingi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BAADHI ya madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba mkoani Kagera, wamewataka watendaji wa halmashauri hiyo kupitia idara ya elimu kuweka uwiano wa walimu wa kike na kiume katika shule zote za msingi na sekondari.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya madiwani wa viti maalumu kutembelea karibu shule zote za msingi na kubaini kuwapo nyingi ambazo hazina walimu wa kike, huku baadhi zikikutwa na mwalimu mmoja tu wa kike wakati zina idadi kubwa ya wanafunzi.

Wakizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani cha kujadili mapato na matumizi ya fedha katika robo ya pili inayoanzia mwezi Oktoba hadi Desemba 2021, madiwani hao walisema kuwa hali hiyo inawatesa watoto wa kike maana wanakabiliwa na mambo mengi kutokana na maumbile yao, ambayo ni vigumu kumweleza mwalimu wa kiume.

Mmoja wa madiwani hao, Zainabu Shakiru, alisema kuwa suala hilo linasababisha watoto wa kike kuathirika kisaikolojia kwa sababu muda wote wanakuwa wamezungukwa na walimu wa kiume na kukosa mtu wa kumweleza matatizo yao kwa uhuru.

"Sisi madiwani tunachoomba kuwapo uwiano wa walimu wa kike na kiume katika shule zote kuanzia za msingi hadi sekondari, kama tatizo ni shule kuwa vijijini, mbona huko kuna watendaji wa vijiji na kata ambao ni wanawake na wanaweza, kwa nini walimu ndio wasiweze," amehoji Joyce Kahangwa Diwani Viti Maalumu.

Akizungumzia suala hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba, Fatna Laay, alikiri kuwapo kwa tatizo hilo na kuahidi kulishughulikia, ili kuwapunguzia athari watoto wa kike zinazotokana na hali hiyo.

"Kuna changamoto kubwa ya uhaba wa walimu kwa ujumla na walimu wengi tulionao ni wa kiume na ndio maana unaweza kukuta kuna shule haina mwalimu wa kike," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa kuna shule zaidi ya 30 hazina walimu wa kike na zote ni za pembezoni, lakini shule nyingi zilizoko mjini na ambazo ziko karibu na mjini zina walimu wengi wa kike.

"Tunafanya utaratibu sasa ili kupunguza walimu wa kike katika shule hizo na kuwapeleka vijijini, lakini changamoto iliyopo shule nyingi zilizoko karibu na mjini, walimu wengi wa kike walioko katika shule hizo ni wake wa wataalamu wanaofanya kazi makao makuu ya mkoa na wengine wana matatizo ya kiafya," alisema.

# Bunge lataka kasi Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote

**Na Salome Kitomari,** DODOMA

BUNGE limeitaka serikali kupeleka bungeni mapema iwezekanavyo Muswada wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote, ili kuharakisha upatikanaji wa huduma hiyo muhimu kwa Watanzania.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, Stanslaus Nyongo, aliyasema hayo bungeni wakati akiwasilisha maoni ya kamati hiyo.

Alisema mpaka sasa asilimia 26 tu ya Watanzania ndiyo wamefikiwa na huduma ya bima ya afya nchini.

Kwa mujibu wa Nyongo, upatikanaji wa huduma za afya kwa wote ni haki ya msingi ya kila mwanadamu, lakini ni utekelezaji wa lengo namba tatu la Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Millenia (SDGs).

Alisema Muswada wa kutunga Sheria ya Bima ya Afya kwa wote umechukuwa muda mrefu kutokana na ugharamiaji wa bima ya afya kwa watu wasio na uwezo asilimia 26.4 kupitia Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), ambalo linahitaji kupata ufumbuzi ndani ya

"Kamati imeelekeza serikali kuhakikisha sheria itakayotungwa ihakikishe kunakuwapo na uboreshaji upatikanaji wa huduma kama dawa, vipimo ili kuepuka usumbufu ambao wananchi wamekuwa wakipata hasa walio katika mfuko wa CHF,"alisema Nyongo.

Aidha, alisema ili kuhakikisha huduma zinaboreshwa, changamoto ya uhaba wa watumishi katika Sekta ya Afya lazima ipatiwe ufumbuzi.

Alisema kamati imeona kuwa sheria iwe wazi kuhusu masuala ya udhibiti na usimamizi, kwa kuanzisha Mamlaka ya udhibiti ya Bima ya Afya badala ya kutumia Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA).

"Serikali ihakikishe kunakuwa na 'ring fenced' budget' ya Mfuko wa Bima ya Afya hasa ikizingatiwa kuwa kuna wengi hawana uwezo ili kuepuka mfuko kufilisika,"alisisitiza.

Pia wizara iendelee kuelimisha na kuhamasisha jamii umuhimu wa kuendelea kupata chanjo ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Aidha, kamati imetaka wizara kuruhusu madaktari bingwa kutumia uzoefu wao kutoa dawa wanazoona zinafaa kwa wagonjwa bila ya kuwapangia.

Kwa upande wa sekta binafsi, alisema "ili kuboresha utoaji wa huduma za afya, sheria itakapokuja, sekta binafsi ziruhusiwe na kuwapo na ubunifu utakaowezesha wananchi kuchagua vifurushi wanavyoona vinafaa."

# Wateja 100 zaidi wazoa mil. 10/- NMB MastaBata

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB jana imechezesha droo ya sita ya kila wiki ya promosheni ya MastaBata-Kivyako Vyako ambapo wateja wake 100 zaidi wamenyakua zawadi za fedha taslimu zenye thamani ya Sh. milioni 10.

Akizungumza kabla ya kuchezeshwa droo hiyo jijini Dar es Salaam, ofisa kutoka Idara ya Kadi, Lightness Zablon, alisema katika droo tano zilizotangulia wateja 500 wameshinda jumla ya Sh. milioni 50.

"Kama watangulizi wao, wateja watakaobahatika kushinda leo kila mmoja wao atashinda pesa taslimu Sh. 100,000. Pia zipo zawadi za Sh. milioni moja kwa kila mteja kwa wateja 25 kila mwezi," Zablon alibainisha.

"Kwenye droo ya mwisho mwezi ujao, wateja 30 watanyakua shilingi milioni 3 kila mmoja," aliongeza.

Kufuatia kutolewa kwa shilingi milioni 10 baada ya droo ya hiyo mwishoni mwa wiki iliyofanyika Makao Makuu ya NMB, jumla ya Sh. milioni 85 zimenyakuliwa na wateja 625 wa taasisi hiyo ya fedha mpaka sasa.

Hiyo inatokana na Sh. milioni 60 za kila wiki pamoja na Sh. milioni 25 za droo moja ya kila mwezi. Zaidi ya wateja 1,000 wa NMB wanatarajiwa kushinda zaidi ya Sh. milioni 200 zilizotengwa na benki hiyo katika msimu huu wa tatu wa kampeni ya MastaBata.

Zablon alisema promosheni ya NMB MastaBata-Kivyako Vyako ilizinduliwa mwishoni mwa mwaka jana kuwahimiza wateja wa benki hiyo kuongeza matumizi ya kadi za malipo za NMB Mastercard na Mastercard QR.

NMB pia inatumia kampeni hii ya kuchagiza maendeleo ya uchumi wa kidijitali kuwazawadia wateja wake waaminifu ambao wamekuwa sehemu muhimu ya mafanikio ya safari yake ya mabadiliko ya kidijitali.

Kwenye droo mbili za mwezi zitakazofanyika wakati wa shindano hili la wiki 10, jumla ya wateja 50 watashinda Sh. milioni 50 wakati wale 30 wa droo ya mwisho watanyakua Sh. milioni 90.

Benki ya NMB ilizindua promosheni ya MastaBata mwaka 2018 ikilenga zaidi kuongeza matumizi ya kadi za malipo kama sehemu yake ya kuunga mkono jitihada za kuifanya Tanzania kuwa uchumi wenye matumizi madogo ya fedha taslimu.

# Vijana wa kike waliosoma sayansi wapewa fursa zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

IKIWA ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Vijana wa Kike waliosomea masomo ya sayansi, Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) imeweka wazi mpango wake wa kuwapa fursa na kuajiri vijana wa kike wanaomaliza vyuo katika fani za sayansi.

Fursa hiyo imetolewa kupitia programu yao inayojulikana kwa jina la STEM (Science, Technology, Engineering, and Mathematics).

Imeelezwa kuwa hatua hii inaambatana na malengo ya kimataifa ya maendeleo endelevu ya Umoja wa Mataifa ya mwaka 2030 yanayolenga kuhamasisha ushiriki wanawake na vijana wa kike kwenye sayansi.

Pamoja na hayo, mpango huu kabambe wa SBL unaendana na mkakati wa Serikali ya Tanzania ya kuongeza idadi ya vijana wa kike kwenye fani za sayansi kwa kujenga zaidi ya shule za sayansi za wasichana kote nchini. SBL imeyasema haya katika taarifa yake kwa vyombo vya habari iliyotolewa jana.

Kwa mujibu was SBL, pogramu ya STEM inalenga kuajiri idadi kubwa ya vijana wa kike wanaotamani kujiunga na kampuni na watafanya kazi kwa muda wa miezi kumi na miwili wakiwa na Shahada ya Kwanza/diploma ya juu au inayolingana na shahada ya kwanza katika fani za uhandisi wa umeme, uhandisi wa kielektroniki, uhandisi wa umekanika, uhandisi wa mitambo, sayansi ya chakula na teknolojia.

Saraphina Mwamaso, msimamizi wa programu hiyo wa SBL alizungumza kwenye warsha iliyohudhuriwa na vijana wa kike waliopo katika fani za sayansi, alisema:

"Tangu kuanzishwa kwa programu hii ya STEM mwaka imeshaajiri vijana kumi wanasayansi wa kike kutoka vyuo mbalimbali Tanzania. Programu hii pia imewainua na kuwaelimisha vijana wa kike kupitia ushauri na mafunzo. Lengo letu ni kuboresha na kuimarisha tofauti za kijinsia katika SBL hasa katika idara ya ugavi."

Mmoja wa wahitimu wa fani ya shahada ya elektroniki na TEHAMA kutoka Taasisi ya Teknolojia ya Dar Es Salaam (DIT), Flora Munuo, alizungumzia uzoefu wake kama mwanafunzi wa STEM, alisema:

"Ni muhimu kutambua mchango wa vijana wa kike katika sayansi kwa sababu ukiwa na ujumuishwaji mkubwa huchangia uvumbuzi zaidi. Kuna idadi kubwa ya vijana wa kike ambao tuna uwezo wa kuvumbua dhana mpya na matumizi. Ninaishukuru sana SBL kwa kutambua uwezo wangu na kunipa nafasi kwenye programu hii."

Rukia Tezura, mhitimu mwingine wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shahada ya Uhandisi wa Mawasiliano alielezea pia uzoefu wake kwa kusema ana imani kijana yeyote wa kike mwenye kipaji katika sayansi anaweza kufanya mambo makubwa sana.

Ni lazima tuwe na ujasiri wa kuchangamkia fursa hizi ambazo zitatuwezesha kupanga safari ya mafanikio katika kupitia programu kama hii ya STEM. Nawaasa vijana wote wa kike mjitokeze na muonyeshe kile mnachoweza, ni matumaini yangu kuwa wasichana wote watayapokea haya kwa furaha," alisema.

Halikadhalika, SBL imesisitiza kuwa mkakati wake wa muda mrefu ni kukuza vipaji vya vijana wa kike kuwa viongozi bora wa baadaye wa kampuni kupitia mafunzo mbalimbali ya kujenga nidhamu na uthamani katika kila kazi ndani ya kampuni.



Baadhi ya wasichana ambao ni wanufaika wa programu ya STEM kwa ajili ya wanaosoma sayansi na wenye uwezo mkubwa darasani inayoendeshwa na Kampuni ya Bia ya Serengeti (SBL) wakinyoosha mkono wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake katika Sayansi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bodaboda waonywa muziki sauti kubwa

**Na Salome Mwasamale**

DEREVA bodaboda hapa nchini wametakiwa kuacha tabia ya kuwasha nyimbo kwa sauti kubwa wawapo barabarani hasa nyakati za kazi asubuhi na usiku kwa kuwa kelele zinachafua mazingira na kuleta kero kwa wananchi.

Akizungumza na Nipashe mwenyekiti wa bodaboda stendi ya kona Mvuti Kata ya Chanika Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, Mohamed Mdogwa, alisema wao wameanzisha utaratibu maalum wa kuwapiga cheni na kuwatoza faini madereva wote watakaoingia katika kijiwe hicho huku wakipiga muziki. Mdogwa alisema wameanza utekelezaji huo katika kijiwe chao lakini nia yao ni kuhakikisha nchi nzima wanaiga mfano huo kwa kuwa kelele zinasumbua wafanyabiashara wengine na wananchi kwa ujumla lakini ni uchafuzi wa mazingira.

"Sisi mtu akikutwa anapiga mziki katika kijiwe chetu anapigwa cheni hadi alipe faini Sh. 3000 ndipo ataruhusiwa kuendelea na kazi vinginevyo tunaifungia pikipiki hiyo na kuiweka yadi huku akiilipia Sh. 1000 kila siku mpaka atakapokuja kuiokomboa,"alisema.

Alisema wanaangalia utekelezaji katika kituo chao utakavyozaa matunda na wakiona inafaa wataandika barua na kuomba vikao katika matawi mengine ili kuliwasilisha hilo ili ikiwezekana na wengine waache tabia hiyo.

Aliongeza kuwa kama mziki ulivyopigwa marufuku katika baa mida ya mchana vivyo hivyo mziki kwa madereva unapaswa kupigwa marufuku kwenye bodaboda kwa kuwa ni kero kwa wananchi hasa nyakati za asubuhi na usiku.

"Utakuta mtu amepakia wanafunzi asubuhi anawapeleka shule lakini kafungulia mziki mpaka mwisho kiasi ambacho hata hao watoto wakipata shida huko nyuma hawezi kujua hivyo hili linapaswa kukomeshwa kabisa," alisema.

Wakizungumzia suala hilo baadhi ya wananchi wa Chanika waliipongeza hatua hiyo na kudai kuwa ni kero kubwa hivyo jitihada hizo zinapaswa kuungwa mkono na serikali ili ikiwezekana waache kabisa tabia hiyo.

Nipashe
Spotika



WACHEZAJI 10 WENYE 'ASISTI' NYINGI DUNIANI UK. 12



Anfield - Liverpool

# VIWANJA VI5 VINARA KWA AMSHAAMSHA MASHABIKI

**LONDON, England**

KLABU ya soka ni nzuri kama mashabiki wao na uwanja ni mzuri kama anga yake. Bila mashabiki kupiga kelele, hata uwanja wa kisasa zaidi wa mpira unaweza kujisikia usio na uhai. Bila kelele za sauti na nyimbo zinazofuatana kutoka kwa mashabiki waaminifu, hakuna timu inayoweza kupata "faida ya kucheza nyumbani".

Leo, tutaangalia viwanja vitano vya soka ambavyo vinaifanya timu kuonekana kama ina wachezaji 12 uwanjani. Viwanja hivi vitano vinaweza visiwe vya bei ghali zaidi, lakini ni jinsi zinavyopambania timu zao.

**#5. Uwanjwa wa Ali Sami Yen Sports Complex NEF - Galatasaray A.S.**

Nyumbani kwa wababe wa Ligi Kuu ya Uturuki, Galatasaray A.S. Uwanja wa Ali Sami Yen Sports Complex NEF ni mojawapo ya viwanja vinavyovutia zaidi barani Ulaya. Mashabiki wa klabu hii kubwa wamejiandaa kwenda kwa kiwango chochote kuishangilia klabu yao hivyo kufanya maisha kuwa magumu kwa timu ngeni.

Wao ni wa kumetameta, wenye sauti kubwa, na wanaweza kuwa na maana ya kipekee kwa upande wa kutembelea, kuhakikisha hakuna dhaifu anayeweza kustawi katika uwanja wao wa nyumbani. NEF, ambayo zamani ulijulikana kama Turk Telekom Arena, uliingia katika Kitabu cha Rekodi za Dunia cha Guinness kwa kuwa uwanja wa mpira wenye sauti zaidi.

Wakati Galatasaray ilipokuwa ikicheza mwaka 2011, mashabiki kwenye uwanja walirekodi sauti ya juu ya desibel 131.76, ambayo bila shaka ilisikika kote jijini.

Uwanja wa NEF, uliozinduliwa mwaka 2011, unaweza kuchukua hadi watu 52,223 katika usiku wa soka. Huku gharama za ujenzi zikifikia Euro milioni 128, uwanja huo umejaa vitu vya kisasa vya usalama.

**#4. Celtic Park - Celtic**

Ligi Kuu ya Uskoti mara nyingi huonekana kama ligi ya farasi wawili, huku Rangers na Celtic zikiwania taji mara nyingi zaidi. Celtic, haswa, imekuwa na mafanikio makubwa katika muongo uliopita, ikishinda taji la ligi kila msimu kati ya 2011 na 2020.

Wamekuwa na baadhi ya wachezaji bora katika safu zao, bila shaka, lakini lazima pia wavue kofia yao kwa Celtic Park kwa usaidizi usio na shaka.

Celtic Park, mojawapo ya viwanja bora zaidi duniani, unajua kila mbinu kwenye kitabu ili kuweka shinikizo kwa wapinzani. Kila mguso unazomewa, kila mchezaji anadhihakiwa. Haiwezekani kustawi kwenye uwanja huu isipokuwa uwe na ngozi nene.

Mbinu zao za kutisha ni nzuri sana, waliweza kuiongoza timu yao kupata ushindi wa kihistoria wa mabao 2-1 dhidi ya Barcelona kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2012-13.

Uwanja wa Glasgow unachukua hadi watu 60,832 na una uwanja maalum wa kusimama kwa mashabiki walio na shauku kupita kiasi. Uwanja huo ulijengwa mnamo mwaka 1888 na kwa sasa una uso wa nyasi asili.

**#3. Diego Armando Maradona Stadium - SSC Napoli**

Timu ya Serie A Napoli iko mbali na kuwa miongoni mwa timu zilizopambwa zaidi nchini Italia. Wameshinda mataji mawili pekee ya Serie A katika historia yao, huku la mwisho likiwa mwaka 1990.

Licha ya uchezaji mdogo, mashabiki wa Napoli hujitokeza kila siku ya mechi, wakishangilia timu yao kwa nguvu zao zote.

Uko katika kitongoji cha Fuorigrotta cha Naples, Uwanja wa Diego Armando Maradona ndio uwanja wa tatu kwa ukubwa. Umepewa jina la mchezaji wao wa zamani, Diego Maradona, una uwezo wa kuchukua watu 54,726, kati ya siti hizo 16,584 ni viti vilivyofunikwa.

Uwanja huo ambao hapo awali ulijulikana kama Stadio San Paolo, unajulikana kwa sauti kubwa, na maonyesho ya moto.

Msimu huu, wana nafasi ya kumaliza ukame wa taji la ligi na hatimaye kurudisha taji hilo nyumbani kwa mara ya kwanza baada ya miaka 22.

**#2. Anfield - Liverpool**

Uwanja wa kupendeza zaidi nchini Uingereza, Anfield, pia unatokea kuwa uliopambwa zaidi kwenye orodha yetu. Kwa hisani ya utamaduni wa soka wa Liverpool, Anfield imeshuhudia timu yake ikisherehekea mataji 19 ya Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Ulaya mara sita, miongoni mwa mengine.

Tofauti na viwanja vingi, uwanja huo wa pale Merseyside hauzingatii kuwadhalilisha wapinzani. Badala yake, unatoa tu upendo usioyumba na usaidizi kwa 'Wekundu' hao.

Anfield, makao ya wimbo maarufu "You'll Never Walk Alone," daima umekuwa kuhusu subira, uvumilivu, na matumaini, hata wakati hakuna kitu kinachoonekana kutokea.

Hakuna mtu aliyeshangaa, kauli mbiu hiyo imeruhusu Anfield kushuhudia mabadiliko mengi. Mechi za hivi karibu kati ya hizo zilikuja dhidi ya Barcelona wakati Wekundu hao walipopindua mabao 3-0 katika mechi ya mkondo wa kwanza kwa kuandikisha ushindi wa ajabu wa 4-0 kwenye Uwanja wa Anfield.

Wakichochewa na ushindi huo maarufu katika nusu-fainali, Liverpool hatimaye walifanikiwa kunyanyua Ligi ya Mabingwa msimu wa 2019-20, kwa kuwalaza Tottenham Hotspur 2-0 kwenye fainali.

**#1. Signal Iduna Park - Borussia Dortmund**

Uwanja wa ajabu zaidi, unaoonyesha hisia, na wa kutisha kabisa barani Ulaya, Signal Iduna Park ya Borussia Dortmund ipo kileleni mwa orodha yetu.

Kwa hisani ya ubabe wa Bayern Munich, Borussia Dortmund hawajapata nafasi ya kushinda mataji mengi hivi karibu, lakini ukame wao umewafanya mashabiki wao kujitolea zaidi. Wanamiminika kila usiku, wakishangilia timu yao, bila kujali ubora wa upinzani.

Ukiwa na uwezo rasmi wa kubeba watazamaji 53,028, Signal Iduna Park sio tu moja ya viwanja vikubwa zaidi barani Ulaya, lakini pia ni wa kipekee. Upande wa kusini wa uwanja ni karibu na jukwaa moja kubwa, lenye uwezo wa kukaribisha mashabiki 24,000.

Upande wa kusini mara zote hukaliwa na wafuasi wakereketwa wa klabu hiyo, ambao huvaa bendera za jadi za njano na nyeusi. "The Yellow Wall" ya Dortmund imekuwa tamasha maarufu katika soka, kitu ambacho hata mashabiki wa Bayern Munich wanakihusudu.

## ISIKUPITE

CHELSEA inakuwa klabu ya tatu England kutwaa ubingwa wa Klabu Bingwa Dunia baada ya Manchester United na Liverpool. Miamba hiyo ya 'Darajani' juzi iliichapa Palmeiras ya Brazil kwa mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Mohammed Bin Zayed huko Abu Dhabi, Falme za Kiarabu.



## Extra Time



Messi

# WACHEZAJI 10 WENYE 'ASISTI' NYINGI DUNIANI

**LONDON, England**

WAKATI wafungaji mabao wakipata sifa nyingi katika soka, juhudi za watengenezaji mabao haziwezi kupuuzwa. Mchezaji ana mzigo wa kuipita ngome ya wapinzani na kufunga.

Ni wachezaji wenye vipaji vya hali ya juu pekee ndio wameweza kuipa timu nafasi ya kufunga mabao kwa kasi inayotakiwa. Ingawa washambuliaji wana kazi muhimu zaidi katika soka, wao si lolote bila watengenezaji mabao ambao wanaweza kuleta mabadiliko katika mchezo.

Wachezaji wote kwenye orodha hii baadhi yao wamekuwa bora zaidi katika miaka ya hivi karibuni, na wameburudisha kwa uchezaji wao wa hali ya juu.

Bila kuchelewa zaidi, wacha tuwaangalie wachezaji 10 wenye pasi nyingi zaidi za mabao ambao bado wanacheza soka hadi sasa...

**#10. Neymar Jr. - 218**

Akiwa na mashabiki wengi duniani kote, Neymar amekuwa mmoja wa wanasoka wenye vipaji vingi zaidi duniani. Mbrazil huyo aliondoka Barcelona mwaka 2017 na kujiunga na PSG kwa kitita cha euro milioni 222.

Miguu ya Neymar mara nyingi imeonekana kuwa mingi sana kwa upinzani kumudu, na anaendelea kufurahisha ulimwengu kwa ustadi wake. Neymar ana jumla ya asisti 218 hadi sasa. Ana mabao matatu na asisti tatu katika mechi 10 za Ligue 1 msimu huu.

Mbrazil huyo amekuwa akisumbuliwa sana na majeraha, yanayomzuia kufikia uwezo wake halisi. Amekumbana na suala kama hilo msimu huu na hajashiriki katika mchezo wowote PSG tangu mwishoni mwa Novemba mwaka jana.

**#9. Franck Ribéry - 248**

Mmoja wa wanasoka bora wa kizazi hiki, Franck Ribery mara nyingi amekuwa akidharauliwa. Ribery aliunda ushirikiano mzuri sana na Arjen Robben kule Bayern na akaendelea kutawala mpira wa ndani na wa Ulaya. Alishinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Mwaka wa UEFA mwaka 2013 na pia alishika nafasi ya tatu kwenye Ballon d'Or, nyuma ya Lionel Messi na Cristiano Ronaldo.

Ribery aliondoka Bayern na kujiunga na Fiorentina mwaka 2019. Kwa sasa ana asisti 248 kwa jina lake. Ribery hakuwa na klabu mwanzoni mwa msimu wa 2021-22, lakini hatimaye alijiunga na 'Salernitana'.

Mfaransa huyo alikuwa muhimu katika ushindi mkubwa wa Bayern katika miaka kadhaa iliyopita. Ameshinda mataji tisa ya Bundesliga, Ligi ya Mabingwa Ulaya moja, mataji sita ya Ujerumani, na mataji manne ya Super Cup akiwa na 'Bavaria' hao.

**#8. Zlatan Ibrahimovic - 255**

Zlatan Ibrahimovic ni mfano halisi wa maneno "kuzeeka kama divai nzuri". Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 40 anaendelea kujituma uwanjani na anaendelea kuvunja rekodi katika klabu ya AC Milan. Ibrahimovic ni mmoja wa wanasoka waliotamba zaidi, akiwa ameshinda mataji zaidi ya 30 katika maisha yake ya soka.

Zlatan pia ndiye mchezaji pekee aliyeshinda mataji 11 ya ligi kwenye ligi nne, yaani Eredivisie (Uholanzi), Serie A (Italia), LaLiga (Hispania), na Ligue 1(Ufaransa). Ibrahimovic kwa sasa ana asisti 255 kwa jina lake. Raia huyo wa Sweden ana mabao manane na asisti mbili kwenye Serie A msimu huu. Hakuna shaka kwamba ataendelea kuongeza idadi hii.

**#7. Cesc Fabregas - 260**

Cesc Fabregas amekuwa mchezaji bora wa kiungo wa kati, haswa wakati wa siku zake za mapema Arsenal. Raia huyu wa Hispania alikuwa na kipaji na alikuwa kiongozi uwanjani. Kwa hakika, Arsene Wenger aliamini uwezo wake kiasi kwamba alifanywa kuwa nahodha wa 'Washikabunduki' akiwa na umri wa miaka 21.

Fabregas alisajiliwa na Barcelona mwaka 2011, hata hivyo, kwa sababu ya uwapo wa nyota Xavi na Andres Iniesta walikuwa wanatawala eneo la kiungo, alipata muda mfupi sana wa kucheza. Fabregas alirejea Ligi Kuu England mwaka 2014 na akasajiliwa Chelsea. Alishinda taji la Ligi Kuu mara mbili, Ligi ya Europa moja, na Kombe la FA moja akiwa na Blues.

Fabregas ana asisti 260 katika maisha yake ya soka hadi sasa. Raia huyo wa Hispania hajacheza vizuri msimu huu kutokana na jeraha la nyama ya paja alilopata Septemba.

**#6. Mesut Özil - 261**

Wachezaji wengi wamekuja na kuondoka, lakini wachache wameweza kuiga umahiri wa Mesut Ozil. Mjerumani huyo anaonekana ana macho nyuma ya kichwa chake kwa jinsi anavyotoa pasi za kuudhi.

Ozil alikaa Real Madrid kwa miaka mitatu na alijiunga na Arsenal mwaka 2013. Amekuwa mmoja wa wachezaji waliosajiliwa vizuri zaidi Arsenal katika muongo mmoja uliopita. Ozil aliunda muunganiko mzuri na Olivier Giroud na Alexis Sanchez kule Arsenal, akitengeneza mabao kushoto, kulia na katikati. Msimu wa 2015-16, Ozil alitengeneza nafasi 146 na kumaliza kampeni hiyo akiwa na asisti 19 na mabao sita.

Ozil ana jumla ya asisti 261 kwa jina lake. Siku zake za mwisho akiwa na 'Washikabunduki' hao aliacha ladha chungu katika vinywa vya mashabiki wengi, kwani aliwekwa kando kutokana na mabishano ya vyombo vya habari. Ozil alijiunga na Fenerbache katika dirisha la uhamisho la Januari mwaka 2021 na kwa sasa ana mabao manane na asisti mbili za klabu hiyo.

**#5. Angel Di Maria - 269**

Angel Di Maria alisajiliwa na PSG mwaka 2015 na amekuwa akitegemewa katika kikosi hicho. Michango ya Di Maria kutoka kwenye winga imekuwa mikubwa na ubunifu wake na maono yanamfanya kuwa mchezaji wa ajabu.

Di Maria ana jumla ya asisti 269 katika maisha yake ya soka hadi sasa. Pia anashikilia rekodi ya kutoa pasi nyingi zaidi katika historia ya PSG. Raia huyo wa Argentina alitoa pasi za mabao 18 katika msimu wake wa kwanza PSG.

Di Maria ana asisti nne na tatu kwenye Ligue 1 msimu huu. Ameshinda kiasi kikubwa cha mataji akiwa na Real Madrid na PSG. Hata hivyo, Ligi ya Mabingwa Ulaya mara zote imekuwa ikiikwepa PSG na atajaribu kupata taji hilo linalotamaniwa sana msimu huu.

**#4. Cristiano Ronaldo - 272**

**Cristiano** Ronaldo aligonga vichwa vya habari aliposajiliwa na Manchester United mwanzoni mwa msimu wa 2021-22. Akiwa na umri wa miaka 37 sasa, wachezaji wengi kwa umri huo huwa wanatundika daluga zao, lakini Ronaldo anaendelea kuvutia.

Mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Ballon d'Or ana jumla ya asisti 272 na ana uhakika wa kuongeza zaidi kwenye mabao yake. Ndiye mwanasoka pekee aliyefunga mabao 800 katika karne hii.

Kurejea kwa Ronaldo Old Trafford hakujaenda kulingana na mpango, na timu yake imekuwa chini ya kiwango kwa muda mwingi wa kampeni za Ligi Kuu. Lakini yeye ni miongoni mwa wafungaji wazuri wa mabao. Ana mabao nane na asisti tatu katika mechi 18 za Ligi Kuu England msimu huu.

**#3. Luis Suarez - 277**

Suarez aliondoka Barcelona mwaka 2020 na kujiunga na Atletico Madrid baada ya kukosana na Wakatalunya hao. Mchezaji huyo wa Uruguay alifunga mabao 21 na kuiongoza klabu hiyo kutwaa taji lao la kwanza la Ligi Kuu ya Hispania tangu 2013.

Ingawa Suarez amekuwa mfungaji mabao hodari, ana sehemu yake nzuri ya kutoa pasi za mabao pia. Suarez ana jumla ya asisti 277 katika maisha yake ya soka hadi sasa. Inasemekana alihusishwa na kurejea kwa mshtuko Ligi Kuu England akiungana tena na Steven Gerrard huko Aston Villa. Hata hivyo, Atletico Madrid walitangaza kutomruhusu kuondoka Januari.

Suarez ana mabao saba na asisti mbili katika La Liga msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, hivi karibuni amefikia rekodi ya ufungaji ya Lionel Messi katika mechi za kufuzu Kombe la Dunia. Wote Messi na Suarez wamefunga mabao 27 katika mechi za kufuzu. Bao pekee la mshambuliaji huyo limeweka hai matumaini ya Uruguay kwenda Kombe la Dunia nchini Qatar.

**#2. Thomas Muller - 283**

Bayern Munich daima imekuwa moja ya timu kubwa barani Ulaya na Thomas Muller amekuwa na jukumu kubwa katika hilo. Muller amekuwa Bayern tangu akiwa kijana na ameshinda kila kitu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, ameshinda mataji 10 ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili, mataji sita ya Ujerumani, na Super saba akiwa na Bayern.

Muller amekuwa na kipaji cha kutengeneza nafasi na ndiye anayeongoza kwa kutoa pasi za mabao Bayern. Muller ametoa jumla ya asisti 283 katika maisha yake ya soka. Mjerumani huyo ana mabao sita na asisti 18 katika mechi 20 pekee za Bundesliga msimu huu.

Muller alivunja rekodi ya Lionel Messi ya kutoa pasi nyingi zaidi za mabao kwa mwaka mmoja kwa kutoa asisti 32 mwaka 2021. Hiyo ni mara saba zaidi ya mchezaji yeyote kutoka ligi tano bora za Ulaya.

**#1. Lionel Messi - 357**

Lionel Messi anachukua nafasi ya kwanza kwenye orodha hii na hiyo haishangazi. Raia huyu wa Argentina amekuwa mmoja wa wanasoka wakubwa ambao ulimwengu umewashuhudia. Mfungaji na muundaji mahiri wa mabao, Messi mara nyingi amekuwa akiibeba Barcelona peke yake kwa miaka 18 aliyokaa na klabu hiyo.

Messi ana jumla ya asisti 357, na inaonekana hakuna mtu atakayemkaribia Muargentina huyo. Messi aliondoka Barca baada ya kucheza mechi 778 kwa Wakatalunya hao na kusaini Paris Saint-Germain mwanzoni mwa msimu wa 2021-22.

Mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon d'Or, amekuwa na wakati mgumu akiwa na PSG na ana bao moja na asisti sita katika mechi 12 za Ligue 1. Messi ameungana tena na Neymar kwa mara nyingine na wawili hao wana uwezo wa kuipeleka PSG kwenye utukufu wa Ulaya wanaoutamani sana.

## Nukuu

"Wasiwasi wangu mkubwa sasa ni kile ulichosoma kuhusu Saka. Mara tu [Pierre-Emerick] Aubameyang alipoondoka, walipaswa kwenda kwa Saka na kusema, 'Hapa kuna mshahara wako wa pauni 50,000 kwa wiki. Huu hapa mkataba wa miaka minne/mitano. Tafadhali usiingie tena katika hili, Arsenal. Mpe mkataba sasa," **Kiungo wa zamani wa Arsenal, Paul Merson akiitaka 'Gunners' kuwahi kumpa mkataba mpya Bukayo Saka.**



"Nina uhakika Kombe la Dunia halitachezwa kila baada ya miaka miwili, kwa sababu ni wazo la kijinga. Inaonekana kwangu kuwa shirikisho la mpira lingekuja na wazo la kupunguza kalenda ambayo wachezaji wanahangaika nayo," **Rais wa Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA), Aleksander Ceferin, akipinga wazo la Kombe la Dunia kuchezwa kila baada ya miaka miwili.**



"[Diogo Jota] alikuwa usajili mkubwa sana na hata Liverpool ilipomnunua unafikiri 'oh, hiyo inavutia'. Ununuzi wa kuvutia, unajiuliza ni wapi atafaa, ataingiaje kwenye safu ya washambuliaji watatu?" **Nguli wa soka wa England, Ian Wright akipendekeza majira ya joto straika mmoja wa Liverpool kuuzwa majira ya joto kumpisha Jota na usajili mpya, Luis Diaz.**



# MABAO MA 5 MAKALI RAUNDI YA 14 LIGI KUU



Lusajo

**Na Adam Fungamwango**

NI wiki ambayo Ligi Kuu Tanzania Bara imesimama kupisha michuano ya kimataifa, pamoja na Kombe la FA.

Wiki iliyopita Ligi Kuu ilikuwa kwenye mshikemshike wa raundi ya 14, ikiwa imesalia raundi moja tu, kukamilika kwa mzunguko wa kwanza.

Ilikuwa ni raundi ambayo imekuwa na matukio mengi yakizungumzwa wiki nzima, hasa lawama kwa waamuzi.

Mashabiki wengi wa soka nchini wameonekana kulalamikia zaidi waamuzi, kuwaongelea na kuacha kuangalia baadhi ya matukio mengine mazuri michezoni yaliyofanywa na baadhi ya wachezaji.

Kuna baadhi ya wachezaji wameonyesha ufundi na umahiri mkubwa wa kupachika mabao, lakini hayakuzunguzwa.

Kwenye makala haya, tunakuletea mabao matano yaliyofungwa kwa umaridadi mkubwa kwenye raundi ya 14 ya Ligi Kuu, twende sasa...

**#1. George Pole - Geita Gold vs Polisi Tanzania**

Ilikuwa ni katika dakika ya 23, alikwenda kupiga faulo nje kidogo ya eneo la mita 18, aliachia shuti kali la juu lililokwenda kushoto kwa kipa Geofrey Mkumbo ambaye alijikuta akiruka kama ushahidi tu.

Lilikuwa ni bao la sita la mchezaji kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, lakini ni la pili kwenye mechi hiyo iliyochezwa Februari 6, mwaka huu katika Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu na kuongoza timu yake kupata ushindi wa mabao 3-1.

**#2. Habib Kyombo - Mbeya Kwanza vs Ruvu Shooting**

Mbeya Kwanza ilipata faulo umbali upatao takriban mita 20 mpaka 25 hivi, ukaenda kupigwa na Habib Kyombo.

Wakati huo tayari Ruvu Shooting ilikuwa inaongoza kwa bao 1-0 na ilikuwa ni dakika ya 50 kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu iliyochezwa Februari 3 kwenye Uwanja wa Azam Complex, Ruvu wakiwa wenyeji.

Kyombo alitandika mkwaju mkali ambao awali wakati anaupiga ulionekana kama unakwenda kushoto kwa kipa Mohamed Makaka, lakini ulipofika karibu ukakatika na kupinda kulia, kitu kilichofanya kipa huyo kupotea maboya, na hata aliporuka ilikuwa ni ushahidi tu, timu hizo zikatoka sare ya bao 1-1.

**#3. Reliants Lusajo - Namungo vs Mtibwa Sugar**

Lilikuwa ni bao lake la nane msimu huu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Huyu ni Reliants Lusajo, straika hatari mzawa kwa sasa kwenye Ligi Kuu. Ilikuwa ni Februari sita, akipachika bao maridadi, akipata pasi kutoka kwa Hashim Manyanya likiwa la kwanza kwenye mechi hiyo. Pamoja na kwamba alikuwa karibu na lango la wapinzani wake, lakini alikuwa eneo gumu la kufunga. Pasi haikuja pia vizuri, alichofanya aliruka juu kidogo, mguu wa kushoto ukiuruka mpira na kuunganisha kwa mguu wa kulia, kitu ambacho kingewashinda mastraika wengi. Baadaye alifunga lingine na kuisaidia Namungo kushinda mabao 3-1, na yeye kukaa kileleni mwa orodha ya wafungaji bora akiwa na mabao tisa.

**#4. Collins Opare - Biashara United vs KMC**

Ilikuwa ni dakika ya 74, wakati huo KMC ilikuwa inaongoza kwa bao 1-0. Opare alipata pasi ndefu kutoka kwa Christian Nzigah, ikamkuta akiwa katikati ya mabeki wawili. Alichofanya aliugusa na kuupeleka upande wa kushoto, na ikampoteza beki mmoja wa KMC, ambaye alirudi kulia kukabana na beki mwenzake, huku mfungaji akiwa upande wa kushoto peke yake. Kabla hawajajua nini cha kufanya, aliachia 'fataki' kali iliyomshinda kipa Juma Kaseja na kujaa wavuni na mechi kumalizika kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.


**#5. Erick Mwijage - Kagera Sugar vs Coastal Union**

Aliuchukua mpira wa pasi ya kichwa, mita chache kutoka katikati ya uwanja. Akiwa kwenye kasi, akifukuzana na beki wa Coastal Union Jackson Shiga, aliupata mpira na kuukokota kwa mita kadhaa hadi karibu na eneo la hatari, akapunguza spidi.

Erick Mwijage alipopunguza spidi, Shiga alimpita na kwenda kwa lengo la kumzuia. Alichofanya Erick na kuanza kuchanganya miguu kama Cristiano Ronaldo, halafu akamdanganya kama anapita kulia. Haikuwa hivyo, ghafla akabadilisha uelekeo na kupita kushoto, na kumchanganya beki huyo akiwa ameshapotea. Hatua moja tu ambayo Erick aliipiga kwa kumpita Shiga aliachia shuti la mguu wa kushoto, lakini halikuwa kali sana, ila la kiufundi, mpira ukajaa ndani ya wavu.

Ilikuwa ni dakika ya 19, likiwa ni bao la kwanza kwenye mechi hiyo iliyochezwa Februari 5, Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera wenyeji wakishinda kwa mabao 2-1.

**JE, WAJUA?**



ZLATAN Ibrahimovic ameungana na Cristiano Ronaldo kuwa wachezaji wawili pekee ambao wamefunga mabao dhidi ya timu tofauti 80 katika ligi tano bora Ulaya tangu mwaka 2000.







Naibu Spika wa Bunge, Mussa Hassan Zungu (kulia), akikabidhiwa zawadi ya ua na Diwani wa Kata ya Kivukoni, Sharik Choughule, ili kumpongeza kwa kuchaguliwa na wabunge kuwa Naibu Spika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mpango ulivyoongeza kasi uandikishaji watoto shule

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amesema Mpango wa Elimumsingi bila malipo umeongeza uandikishaji wanafunzi ambapo kwa mwaka huu wanafunzi 3,046,919 wameandikishwa elimu ya awali, msingi na sekondari.

Bashungwa aliyasema hayo juzi jijini hapa kwenye hafla ya utoaji wa Tuzo za Ubora wa Taaluma kwa matokeo ya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi, kidato cha nne na kidato cha sita kwa mwaka 2021 iliyodhaminiwa na Chama Cha Walimu Tanzania (CWT).

Alisema tangu kuanza kutekelezwa kwa mpango huo mwaka 2015, mpaka sasa, serikali imepeleka Sh. trilioni 1.43, kwa ajili ya kugharamia Elimumsingi bila malipo.

"Mpango wa Elimumsingi bila malipo umeleta fursa ya upatikanaji wa elimu kwa kuongeza uandikishaji wa wanafunzi, kutokana na kuondolewa kwa vikwazo, katika mwaka 2016, jumla ya wanafunzi 2,670,125 waliandikishwa, kati ya hao wanafunzi 917,137 wa elimu ya awali, 1,386,592 wa darasa la kwanza na wanafunzi 366,396 wa kidato cha kwanza," alisema.

Alibainisha kwa mwaka 2022, jumla ya wanafunzi 3,046,919 wameandikishwa, kati ya hao wanafunzi 1,123,800 ni wa elimu ya awali sawa na asilimia 82, wakiwamo wenye mahitaji maalum 2,352, wanafunzi 1,454,544 ni wa darasa la kwanza sawa asilimia 91, na wanafunzi 664,698 wa kidato cha kwanza wameripoti shuleni, sawa na asilimia 73.2 ya wanafunzi waliochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwaka 2022.

Waziri huyo alisema serikali imefanya jitihada kubwa kuongeza miundombinu ya shule kupitia programu na miradi mbalimbali inayotekelezwa nchini ikiwa ni jitihada za kuboresha sekta ya elimu.

Aidha, alisema serikali imepeleka fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya ujenzi wa shule mpya 235 za kata na shule 10 za kitaifa za wasichana za mikoa kupitia mradi wa SEQUIP.

"Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji katika shule za msingi na sekondari nchini lwa mwaka 2021 ufaulu katika mtihani wa kumaliza elimu ya msingi umefikia asilimia 81.97, mtihani wa kumaliza kidato cha nne umefikia asilimia 87.30 na kidato cha sita asilimia 99.62, ninawapongeza kwa kuongeza na kuimarisha ufaulu. Hata hivyo, nina wahimiza kuongeza usimamizi wa shughuli za elimu na kuondoa changamoto zinazosababisha baadhi ya shule kutofanya vizuri," alisema.

Aliagiza kuhakikisha wanafuata sheria, miongozo na taratibu katika usimamizi wa sekta ya elimu ili kufikia malengo ya serikali.

# Serikali na UNICEF kupitia hali ya watoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) limesema lipo tayari kushirikiana na serikali kufanya mapitio ya hali halisi ilivyo sasa kwenye utekelezaji wa maendeleo na ustawi wa watoto.

Mwakilishi Mkaazi wa UNICEF nchini, Shalini Bahuguna, aliyasema hayo jijini hapa alipofanya mazungumzo na Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maaalum, Dk. Dorothy Gwajima, alipofika kujitambulisha na kuonyesha utayari wa kufanya kazi na serikali.

Alisema UNICEF iko tayari kushirikiana na serikali na kwa pamoja watakuja na mkakati unaojibu mahitaji ya wakati wa sasa ili kutimiza matarajio ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa upande wake, Dk. Gwajima alisema wizara hiyo iko tayari kufanya kazi nashirika hilo hasa kwa kuzingatia vipaumbele vya nchi katika mambo ya ustawi na maendeleo ya jamii ya kitanzania.

"Nimekuwa nikifanya ziara za kikazi mikoani na kukutana na kamati za ulinzi wa wanawake na mtoto ngazi ya kata na mitaa ambapo, kilio chao kikubwa ni upungufu wa wataalamu wa maendeleo na ustawi wa jamii kwenye ngazi hiyo, hivyo sisi tunayo imani kupitia ushirikiano wenu changamoto hii itapata ufumbuzi," alisema.

Dk. Gwajima alisema wanatambua na kuheshimu kazi ambayo imeendelea kufanywa na shirika hilo nchini hususan katika ulinzi wa mtoto kabla ya kuundwa kwa wizara hiyo mpya.

# TAWLA yajitosa udhibiti vifo vya uzazi

**Na Ibrahim Joseph, DODOMA**

CHAMA cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), kimejipanga kutoa elimu ya afya ya uzazi nchini ili kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Mratibu wa TAWLA, Wakili Josephine Arnold, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifungua mkutano wa siku moja wa wadau wa afya na sheria kutoka taasisi na wizara mbalimbali uliofanyika jijini hapa.

Arnold alisema TAWLA pamoja na kutoa masada wa kisheria pia inaendelea na utaratibu wa kutoa elimu ya afya ya uzazi hapa nchini kwa lengo la kuwasaidia jamii kutambua umuhimu wa suala hilo.

Alisema TAWLA inatekeleza mradi wenye lengo la kuboresha afya ya uzazi kwa wanawake wenye umri wa uzazi uitwao (Advancing SRHR for women of reproductive age in Tanzania) ambao unakusudia kuchangia na kuboresha afya hiyo ili kuwa na mazingira rafiki ya kijamii, sera na sheria zinazozingatia afya ya uzazi.

Aliongeza kuwa mradi huo unalenga kuongeza uelewa kwa jamii katika masuala ya afya ya uzazi na kuimarisha uwezo wa serikali za mitaa kwenye baadhi ya mikoa.

Aliwataja walengwa katika kuhakikisha kwamba mradi unaleta matokeo tarajiwa, mradi huo unahusisha wadau mbalimbali wakiwamo wanawake na mabinti.

"TAWLA ni shirika lisilo la kiserikali, lisilojiendesha kwa faida, na lililojikita katika masuala ya haki za binadamu hususani haki za wanawake kwa kutoa msaada wa kisheria kwa wanawake na watoto wasio na uwezo kifedha,"alisema.

Aliitaja kazi nyingine kuwa ni kufanya utafiti na utetezi, kutetea utawala bora, uwajibikaji na kuleta usawa wa kijinsia.

Kwa upande wake, Mhadhiri Msaidizi wa Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI) na mwanachama wa TAWLA, Wakili Penina Manyanki, alipongeza serikali pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa juhudi za kuendelea kupunguza vifo vya wanawake vitokanavyo na uzazi.

Alisema hata takwimu zinaonyesha kwa sasa ni vifo ni 556 kati ya vizazi hai 100,000 kwa mwaka.

Kadhalika alisema katika kuunga mkono juhudi mbalimbali za kukabiliana na tatizo hilo TAWLA imeendelea kutoa mafunzo na semina yenye lengo la kuongeza uelewa kwenye Jamii ili kupunguza tatizo hilo.





# Barabara iliyosombwa mafuriko yakarabatiwa

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Mkoa wa Songwe, imeanza kuijenga upya barabara inayounganisha kata za Kanga na Ifwenkenya wilayani Songwe ambayo ilisombwa na mafuriko mwaka jana na kukata mawasiliano kati ya kata hizo.

Akizungumza wakati wa kukagua ujenzi wa barabara hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Simon Simalenga, alisema hatua ya kuanza kuboresha barabara za ndani za wilaya hiyo inatokana na ongezeko la fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Alisema ofisi yake itahakikisha inasimamia kwa nguvu mradi huo pamoja na miradi mingine inayotekelezwa ndani ya wilaya hiyo ili kuhakikisha inatekelezwa kwa viwango vinavyostahili kwa mujibu wa taratibu.

"Tunaishukuru serikali imeongeza fedha kwa ajili ya miradi ya barabara ndani ya wilaya yangu, sisi kama serikali tutahakikisha tunasimamia kwa nguvu zote miradi hii ili fedha zinazotolewa ziwasaidie wananchi," alisema Simalenga.

Aliitaka TARURA kuhakikisha wanakamilisha mradi huo kwa wakati ili wananchi waendelee kunufaika kwa kusafirisha mazao na bidhaa mbalimbali kwenda kuuza kwenye masoko ya ndani na nje ya wilaya hiyo.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Songwe, Mhandisi Kilian Haule, alisema licha ya mvua inayoendelea kunyesha sasa hivi atahakikisha barabara hiyo inakamilika ndani ya muda mfupi na kwa kiwango kinachostahili kwa mujibu wa mkataba.

Alisema lengo ni kuhakikisha mradi huo unaanza kufanya kazi kabla ya Juni mwaka huu wakati ambapo wakulima huwa wanasafirisha zaidi mazao yao.

# Mbaroni madai ya kukodiwa kufanya mauaji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linamshikilia, Bahati Nduta (24), mkazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, kwa tuhuma za kuwa kinara kuua watu kwa kukodiwa.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi Ulrich Mate, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari hukusu msako wa watuhumiwa wa mauaji ya watu hivi karibuni.

Alisema kijana huyo alikodiwa na ndugu wa marehemu, Mkwaya Mwaibanje (65), mkazi wa Kitongoji cha Nkunga katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe ili amuue kutokana na mgogoro wa mashamba uliokuwapo baina ya wana ndugu hao.

Alisema kijana huyo alikubali na kwenda kutekeleza mauaji hayo Novemba 28, mwaka 2020, ambapo alimuua mzee Mwaibanje kwa kumkata na shoka puani na kisogoni akiwa shambani mwake akiendelea na shughuli zake.

Alisema baada ya mtuhumiwa kutekeleza tukio hilo alitoroka na kutokomea kusikojulikana, hali iliyosababisha baadhi ya ndugu wa marehemu waliomkodi kukamatwa na kutiwa ndani mpaka atakapopatikana muuaji.

"Tumemtafuta kijana huyo kwa zaidi ya mwaka sasa, tuliendelea kumsaka taratibu na ilipofika Februari 9, mwaka huu, saa 11:00 alfajiri tulifanikiwa kumkamata akiwa Mbalizi," alisema Kamanda Matei.

Aliwataja ndugu wa marehemu waliomkodi mtuhumiwa huyo ni Mawazo Elisenjeli, Sijaona Mwaibanje na Elijeseli Mwaibanje ambao walikamatwa na kufikishwa mahakamani na kukiri kuwa walimkodi mtuhumiwa huyo kutekeleza mauaji hayo.

Alisema wanaendelea na upelelezi ili kubaini matukio mengine ambayo kijana huyo ameshiriki pamoja na kubaini endapo kuna wenzake anaoshirikiana nao ili hatua zaidi zichukuliwe ikiwamo kufikishwa mahakamani.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kumuua Ofisa Ustawi wa Jamii wa Mahabusu ya Watoto iliyoko Kabwe jijini Mbeya, Glory Kibra (38), kwa kumkaba shingoni.

Kamanda Matei aliwataja watuhumiwa wanaoshikiliwa ni Nicolous Amani (18) ambaye ni miongoni mwa vijana waliokuwa wanalelewa kwenye mahabusu hiyo na Banda Mweupe (45), ambaye alikuwa mlinzi wa mahabusu hiyo.

Alisema watuhumiwa walitekeleza mauaji hayo Februari 3, mwaka huu, ambapo walimvizia marehemu nyumbani kwake saa 3:00 usiku na kumkaba shingoni mpaka kumuua.

Alisema watuhumiwa walipohojiwa walikiri kumuua Ofisa Ustawi wa Jamii huyo kwa lengo la kujipatia mali mbalimbali ikiwamo simu, kompyuta mpakato alizokuwa anamiliki pamoja na fedha za vikundi vya wanawake ambazo alikuwa anakusanya.

"Huyu Nicolous ni miongoni mwa vijana wadogo wanaokabiliwa na kesi za mauaji, alishafanya mauaji huko Rungwe ndipo akaletwa pale sasa alibaini kuwa yule mama alikuwa amekusanya fedha za vikundi mbalimbali vya wanawake wafanyakazi wa ile mahabusu, kwa hiyo akamshawishi mlinzi washirikiane," alisema Matei.

Alisema katika msako ambao jeshi hilo lilifanya katika maeneo mbalimbali ya mahabusu hiyo, walibaini watuhumiwa hao walitelekeza kompyuta na simu walizoiba kwa marehemu kwenye moja ya mabanda ya kuku.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na waandishi wa habari juzi (hawapo pichani), kuhusu utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ndani ya mkoa huo, ambapo alitahadharisha wazazi na walezi ambao watoto wao hawajaripoti shuleni mpaka sasa. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wazazi matatani kukaidi kupeleka watoto sekondari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imetahadharisha kuanza kuwachukulia hatua za kisheria wazazi na walezi ambao wamekaidi kuwapeleka shule wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na masomo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliyasema hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la awali, darasa la kwanza na kidato cha kwanza.

Homera alisema katika baadhi ya maeneo ya mkoa huo hasa Wilaya ya Mbarali idadi kubwa ya wanafunzi bado hawajaripoti shuleni kutokana na visngizio mbalimbali vikiwamo vya kata zao kutokuwa na shule.

Aliwataka wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kuhakikisha wanaripoti kwenye shule walizopangiwa kabla ya Machi Mosi mwaka huu na kwamba baada ya hapo hatua zitaanza kuchukuliwa kwa wazazi pamoja na wanafunzi wenyewe.

Alisema katika wilaya ya Mbarali kuna baadhi ya kata ikiwamo Kata ya Luhanga ambayo ipo ndani ya mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kwa mujibu wa Tangazo la Serikali namba 28 (GN.28) ya Mwaka 2008 hazina shule za sekondari hivyo wanafunzi wamepangiwa kwenye kata jirani.

Alisema wanafunzi wa kata hiyo wamepangiwa kwenda katika Shule ya Sekondari ya Kata ya Utengule-Usangu lakini wengi wao hawajaripoti kutokana na visingizio mbalimbali na hivyo akawataka kuripoti haraka kabla hatua hazijaanza kuchukuliwa.

"Nimeshaiagiza Halmashauri ya Mbarali kuboresha bweni lililoko katika Shule ya Sekondari Utengule-Usangu kwa ajili ya watoto wanaotoka Kata ya Luhanga, kwa hiyo hakutakuwa na kisingizio chochote, lakini hata wengine ambao hawajaripoti naagiza waripoti haraka sana," alisema Homera.

Alisema katika maeneo yote ya mkoa huo yenye migogoro ya mipaka na hifadhi, serikali haifanyi maendeleo yoyote mpaka mipaka migogoro iliyopo itakapokuwa imetatuliwa na kwamba endapo wananchi wataruhusiwa kuendelea kuishi miradi itapelekwa.

Katika hatua nyingine, Homera aliwataka wanafunzi wote walioacha shule kwa sababu mbalimbali ikiwamo kupata mimba warejee shuleni kutokana na serikali kuanzisha mpango maalumu wa kuwasaidia kutimiza malengo yao.

Alisema mpaka sasa wanafunzi waliorejea shuleni baada ya kujifungua wapo 197 na kwamba wanaendelea na masomo katika shule mbalimbali zilizotengwa kwa ajili ya kundi hilo maalumu.

"Nilitembelea Shule ya Sekondari ya Kutwa ya Kyela na kuzungumza na baadhi ya mabinti ambao wamerejea shuleni baada ya kujifungua, wengi wana ndoto nzuri sana na mmoja wapo anasema anataka kuwa mwanasheria," alisema Homera.

Alisema kwa wale ambao hawajarejea, lakini wanatamani kurejea ni vizuri wakarejea ili wanufaike na mpango huo maalumu ulioanzishwa na serikali kwa ajili ya kuwasaidia kutimiza malengo yao.



# Serikali kuimarisha huduma Mnazi Mmoja

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema itaendelea kuimarisha huduma zinazotolewa katika Hospitali Kuu ya Mnazi Mmoja na kutekeleza malengo ya kujenga hospitali ya rufani na kufundishia katika eneo la Binguni pamoja na hospitali za wilaya katika mikoa yote Unguja na Pemba.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo katika hafla ya uzinduzi wa mradi wa kuimarisha huduma za majisafi na salama pamoja na chumba cha kuhifadhia maiti, katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar.

"Ujenzi wa Hospitali ya Binguni, hospitali ya mkoa eneo la Lumumba pamoja na hospitali za wilaya utaipunguzia mzigo Hospitali ya Mnazi Mmoja, hivi sasa wananchi wanalazimika kufuata huduma katika hospitali hii hata kwa huduma za tiba ambazo si za rufani," alisema Rais Mwinyi.

Aidha, Rais Dk. Mwinyi alisema kuwa miradi yote ya ujenzi wa hospitali za wilaya imeshaanza na inaendelea kwa kasi na dhamira ya serikali ni kuona kwamba hospitali hizo zinakamilika na zinazinduliwa mwaka huu.

Dk. Mwinyi pia alitumia fursa hiyo kumpongeza mwekezaji mzalendo Mohamed Abdallah Mohamed, Mkurugenzi Mtendaji wa Zanzibar Cable TV kwa kujitolea kujenga jengo la kuhifadhia maiti katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

"Juhudi za mwekezaji huyu zinachochea ari na hamasa ya wafanyabiashara wenzake na wananchi wengine kujitokeza kutoa misaada kwa jamii. Na hii unadhihirisha usemi usemao mjenga nchi ni mwananchi," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema kuwa hospitali hiyo ilijengwa zamani na mahitaji yake yalizingatia mahitaji halisi ya wananchi kwa wakati huo ambapo jengo la kuhifadhia maiti nalo lilikuwa na uwezo mdogo wa kuhifadhi maiti sita pekee.

"Msaada huu wa chumba cha kuhifadhi maiti chenye majokufu ya kuhifadhia maiti 20 tunauthamini sana pia naipongeza Taasisi ya Lady Fatema Foundation kwa msaada wake wa huduma ya maji katika hospitali hii ya MnaziMmoja," alisema.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kuwa jengo hilo la kuhifadhia maiti lina majokofu ya kisasa yenye uwezo wa kuhifadhi maiti 20, pamoja na sehemu ya kuoshea maiti, sehemu ya kufanya uchunguzi wa maiti na vyumba vya kutoa huduma mbalimbali.

Naye mwekezaji mzalendo Mohamed Abdallah Mohamed alieleza ushirikiano aliopata katika ujenzi wa mradi wa chumba cha kuhifadhia maiti na kuahidi kuendelea kujenga sehemu kwa ajili ya kubadilishia nguo kwa wafanyakazi wa chumba hicho.




Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, ambaye ni mwanzilishi wa gazeti la Zanzibar Leo akiangalia mwonekeno mpya wa gazeti hilo baada ya uzinduzi uliofanywa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), katika sherehe za kutimia miaka 20, jana. **PICHA: IKULU**

# Kituo cha daladala sasa afueni kwa wananchi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, amesema kukamilika kwa kituo cha daladala Kibweni kutarahisisha shughuli za wananchi hususani wagonjwa wanaofika kupata matibabu katika Hospitali ya Kikosi cha Kuzuia Magendo KMKM, Kibweni Zanzibar.

Waziri huyo alisema hayo wakati akikizindua rasmi kituo hicho cha Kibweni kilichofungwa kutumika kwa takribani miaka minne iliyopita kutokana na sababu za kiusalama kwa eneo la kambi ya kikosi hicho.

Alieleza kwamba, Wizara ya Ujenzi imefurahishwa na hatua iliyochukuliwa na kikosi hicho chini ya uongozi wa mkuu wa kikosi hicho, Komodoo Azani Msingiri, ya kuzungushwa ukuta katika eneo hilo sambamba na kuweka miundombinu maalum kwa ajili ya abiria.

Aidha, Waziri Rahma aliwaagiza viongozi kutoka wakala wa barabara pamoja na Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani kuchukua hatua za haraka kuweka alama kwa watu wanaovuka katika eneo hilo.

Kutokana na kufunguliwa kwa kituo hicho Waziri Rahma alitangaza kufungwa kwa kituo cha Bububu Silva kilichokuwa kikitumika kwa dharura.

Naye Mkuu wa Kikosi cha KMKM, Azani Hassan Msingiri, alisema kikosi hicho kimeamua kuchukua hatua ya kukirejesha kituo hicho ili kuwapunguzia wananchi wanaofika kupata huduma ya matibabu katika hospitali hiyo kutembea mwendo mrefu.

Alieleza kuwa kikosi chake ni rafiki mwema kwa wananchi hivyo watahakikisha wanakuwa karibu na wananchi katika kutoa huduma mbalimbali kwa maendeleo ya taifa.

# Othman asisitiza ushirikiano kwa viongozi wapya wa ACT

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha ACT- Wazalendo Zanzibar, ambaye ni na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wanachama wa chama hicho kuendelea kuwaunga mkono viongozi waliochaguliwa hivi karibuni kwa kuwa wamechaguliwa kwa njia ya haki na demokrasia.

Othman ametoa kauli hiyo Gombani ya Kale, Pemba, alipowasili baada ya mapokezi na kutambulishwa rasmi kwa viongozi wa chama hicho walichaguliwa kwenye mkutano mkuu maalum jijini Dar es Salaam, mwezi uliopita.

Aidha, aliwataka wanachama kutosikiliza kauli za baadhi ya viongozi waliopoteza mwelekeo kutokana na tamaa na kusisitiza kwamba amani ya Zanzibar itajengwa na Wazanzibari wenyewe. Alisema kuwa wajumbe wa mkutano mkuu wa chama hicho walichambua kwa kina sifa za wagombea wote waliooomba nafasi za mwenyekiti, makamu mwenyekiti pamoja na mjumbe mmoja wa Halmashauri Kuu Taifa na kwamba waliochaguliwa ndio waliokuwa na sifa zaidi na kupewa ridhaa na wanachama ya kushika dhamana hizo.

Naye Mwenyekiti wa chama hicho Taifa, Juma Duni Haji, aliwaahidi wanachama hao kwamba atatumikia kwa moyo nafasi aliyopewa na wanachama katika jitihada za kuendeleza maridhiano ya kitaifa ujenzi wa demokrasia na utetezi wa haki za binadamu.

Naye Kiongozi wa Chama hicho, Zitto Kabwe, alisema chama hicho kimo katika serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) kwa dhamira njema ya kujenga umoja na maridhiano ya kweli ndani ya Zanzibar.

Alisema chama hicho kinafahamu yapo baadhi ya mambo yaliyokubaliwa kutekelezwa kwenye maridhiano hayo lakini hayatekelezwi ila chama hicho kinaendelea kuyafanyia kazi.

"Serikali ya Umoja wa Kitaifa inapaswa kuwa na faida kwa watu wote na haipaswi kutengeneza mazingira ya kuhalalisha upande mmoja kutawala bali ni kuwapo Zanzibar yenye mamlaka kamili," alisema.

Aidha, alisema Tanzania bado inachangamoto kubwa ya maendeleo ya kiuchumi kwa kutokuwapo ajira, kupanda kwa gharama za maisha ya wananchi na kwamba ACT itaendelea kupigania haki ya wanyonge kupitia uchaguzi huru, tume huru ya uchaguzi pamoja na katiba mpya ya Tanzania.

# Makosa usalama barabarani, maadili yalivyoshtua Bunge

**Na Salome Kitomari, DODOMA**

BUNGE limeshtushwa na ongezeko la makosa ya usalama barabarani na dhidi ya maadili ya jamii, na kutaka hatua madhubuti kuchukuliwa.

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama, kwa niaba ya Mwenyekiti, Vita Kawawa, alisema walibaini idadi ya makosa dhidi ya binadamu yamepungua kwa asilimia 6.1 ikilinganishwa na mwaka 2020.

Alisema makosa dhidi ya maadili ya jamii ikiwamo matumizi ya dawa za kulevya yameongezeka kwa asilimia 29.2 ikilinganishwa na mwaka 2020 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba;

"Makosa haya yakiendelea kuongezeka yanachangia pia ongezeko la makosa dhidi ya binadamu yakiwamo mauaji, kubaka, na kulawiti, hali ambayo si nzuri kwa usalama wa raia," alisema na kuongeza:

"Bunge linaishauri serikali kuwa na mpango mkakati wa kupunguza makosa dhidi ya maadili ili kupunguza matukio ya makosa dhidi ya binadamu ambayo yanaleta taharuki katika jamii na kuathiri usalama wa raia ambao ndio nguzo muhimu ya maendeleo."

Aidha, Kawawa alitaka kuwepo mkakati wa kuboresha vitendea kazi vya kiteknolojia kama vile kompyuta na mifumo mbalimbali, ili kwenda sambamba na kasi inayokusudiwa ya uzalishaji wa vitambulisho vya taifa.

Pia alisema bunge limeona ni muhimu serikali ikatenga fedha za maendeleo kulingana na mahitaji halisi ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ikiwamo kutengewa fedha za kutosha kwa ajili ya manunuzi ya kadi ghafi na ununuzi wa vyombo vya usafiri.

Pi alitaka serikali kutoa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa wakati kwa ajili ya uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa.

"Uzalishaji wa Vitambulisho vya Taifa umeendelea kuwa changamoto ya muda mrefu, hivyo kufanya upatikanaji wa vitambulisho hivyo kuwa chini ya lengo tangu kuanza kuzalishwa kwake mwaka 2013. Kutokuwa na Vitambulisho vya Taifa kunaathiri upatikanaji wa huduma mbalimbali zinazohitaji raia kuwa kama hati ya kusafiria," alisema.



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC) Salim Abri Asas (kulia) , akimkabidhi Mwenyekiti wa UVCCM tawi la Chuo Kikuu cha Iringa, Daud Lukanguji, Sh. milioni 5 ambazo alichangia kupitia mnada wa keki iliyoandaliwa na UVCCM tawi hilo ili kuboresha mfuko wa kusaidiana chuoni hapo. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Kituo utafiti chasikitishwa mboga, matunda kutoliwa

**Na Mwandishi Wetu, ARUSHA**

KITUO cha Utafiti wa Mazao ya Mboga Duniani (World Vegetable) tawi la Tanzania, kimeeleza kutoridhika kwake na tabia ya wananchi katika ukanda wa Mashariki na Kusini mwa Afrika ya kutokula mboga na matunda, tabia ambayo inahatarisha afya zao, na hasa afya za watoto kwa kukosa milo kamili.

Akizungumza katika mahojiano maalumu na waandishi wa habari ofisi kwake jijini hapo jana, Mkurugenzi Kanda ya Mashariki na Kusini mwa Afrika wa World Vegetable Centre, Dk. Gabriel Rugalema, amesema kituo chake kina jukumu la kutafiti na kueleza umuhimu wa matumizi ya mboga na matunda kwa lengo la kulinda na kuimarisha afya ya binadamu.

Amesema utafiti unaonyesha kuwa Afrika uzalishaji na ulaji vyakula vya wanga ni mkubwa mno, lakini watu hawajali kula mboga na matunda kwa hiyo kukosa milo kamili.

"Mikakati tuliyonayo ni kuhakikisha utafiti katika uzalishaji wa mbegu unaongezeka ili kutoa nafasi kwa watumiaji kupata mbegu bora ili wapate mazao mengi, wale mboga na pia kujiongezea kipato kwa kuuza mazao hayo," amesema Dk. Rugemala.

Alisema mboga ina mchango mkubwa katika kuimarisha afya ya binadamu na kwamba ulaji wa mboga unatoa kinga kwa mwili wa binadamu asishambuliwe na magonjwa mbalimbali.

"Tatizo ni kwamba watu wanakula kwa wingi vyakula vya asili ya wanga na kutojali kula mboga na matunda. Kuna haja ya tabia hii ikabadilika haraka kunusuru afya za mamilioni ya watu, hasa watoto."

Mazao ambayo kituo hicho kinayafanyia utafiti ni pamoja na nyanya, biringani, pilipili, bamia, roselle na amaranth.

Ameeleza kuwa kituo hicho kilianzishwa na watu wa bara la Asia mwaka 1971, kwa kufanya utafiti wa mboga kutokana na Afrika kuzalisha na kula mazao ya wanga kwa kiasi kikubwa tofauti na ulaji wa mboga na matunda.

"Tumeanza kufanya utafiti wa mbegu za mazao ya viungo. Mazao haya yana soko kubwa ndani na nje ya nchi. Soko ni kubwa likilinganishwa na upatikanaji wa mazao hayo," amesema Dk. Rugalema na kuongeza:

"Ulimaji wa mazao hayo ni fursa kwa wajasiriamali wadogo na wakati kukuza biashara zao. Ulimaji mkubwa na wa umakini wa mboga na matunda utaibua ajira nyingi kwa wananchi."

Amesema kituo chao kinapata ushirikiano mkubwa kutoka serikani na wadau wengine wa kilimo kama Kituo cha Kuendeleza Kilimo Nyanda za Juu Kusini mwa Tanzania (SAGCOT), katika kuhakikisha mbegu bora za mboga na matunda zinapatikana.

Juma lililopita SAGCOT na Taasisi ya Alliance for a Green Revolution in Africa (AGRA) zilishirikiana kuendesha mafunzo kwa wadau wa mbegu kwa lengo la kuinua kilimo nchini Tanzania na kunyanyua kipato cha wakulima.

## Faidika yazindua huduma ya LetsGo-kidigitali zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

WATEJA wa Taasisi ya kifedha ya Faidika wameboreshewa huduma, baada ya kuzinduliwa mfumo wa kisasa wa kidigitali ujulikanao LetsGo Digital Mall.

Mkurugenzi Mkuu wa Faidika Microfinance Tanzania, Baraka Munisi, alisema kuwa, wamefikia hatua hiyo ili kumwezesha mteja wao kupata huduma bora kwa njia rahisi na haraka zaidi.

Munisi alisema kuwa kupitia LetsGo Digital Mall, mteja anaweza kupata mkopo mpya, kuongeza mkopo, taarifa za akaunti na huduma nyinginezo kwa njia ya simu ya mkononi kupitia USSD namba *149*06#, mitandao na 'App' ya LetsGo powered by Letshego. Kwa mujibu wa Munisi, huduma ya LetsGO Digital Mall itatumika kama kichocheo cha kuwafikia wateja wengi ili kupata huduma za kisasa bila kutembelea ofisi zao.

"LetsGo Digital Mall ni jukwaa linalozingatia wateja na lenye kurahisisha mtumiaji kupata huduma mbalimbali kwa wakati muafaka bila ya usumbufu wowote. Kupitia LetsGO Digital Mall, wateja wetu watapata huduma bora zaidi za kifedha kwa kuzingatia falsafa ya LetsGo Nation bila ya usumbufu wowote katika wakati na eneo muafaka," alisema Munisi.

Mwenyekiti wa Bodi ya Faidika Microfinance Tanzania, Adam Mayingu, alisema kuwa huduma hiyo ni jukwaa bora kwa sasa na wakati ujao hasa kwa njia ya kidigitali.

Mayingu alisema wametumia teknolojia ya hali ya juu ili kufanikisha huduma hiyo na lengo kuu ni kuwanufaisha na kuwaondolea wateja wao usumbufu. Alifafanua kuwa huduma yao ya kigitali inadhihirisha jinsi gani walivyokuwa mstari wa mbele katika kuwajali wateja wao katika huduma za kifedha.

"Tunajisikia fahari kubwa kuwekeza shughuli zetu kwa Watanzania na kuwapa huduma bora kwa njia ya kidigitali zaidi," alisema Mayingu.

Alifafanua kuwa uwekezaji wa kidigitali unasaidia kuongeza viwango vya huduma bora katika huduma mbalimbali. "LetsGo" ni huduma mpya katika katika taasisi yetu yenye lengo la kuleta mageuzi ya huduma za kidigitali hapa nchini na kimataifa," alisema.

Alisema ni fursa kwa wafanyabiashara na wajasiriamali kutumia huduma hii mpya ili kufikia malengo yao. "FaidikaMicrofinance inawaalika watu wote kujiunga na huduma ya LetsGoNation yenye lengo la kuleta mapinduzi ya kidigitali kwa Waafrika wenye lengo la kusaidia kukua kwa uchumi," aliongeza.

# Usikilizaji rufani ya Sabaya kuanza

**Na Allan Isack, ARUSHA**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Arusha, leo itakaposikiliza rufani ya kesi ya jinai namba 105 iliyokuwa inamkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake wawili.

Sabaya kupitia kwa mawakili wake, walikata rufani kupinga hukumu ya kutiwa hatiani na kufungwa miaka 30 kwenda jela na hakimu aliyekuwa akisikiliza kesi hiyo.

Oktoba 15, mwaka mwaka 2021, Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Odira Amworo, alimtia hatiani Sabaya na wenzake kwa kutenda makosa matatu likiwamo la unyang'anyi wa kutumia silaha.

Katika rufani hiyo, mawakili wa utetezi, waliwasilisha hoja 14 kupinga hukumu iliyotolewa na Amworo, kwa kuwa hawakuridhika nayo.

Desemba 13, mwaka jana, Naibu Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Arusha, Ruth Massam, alisema kuwa rufani hiyo namba 129 ilikwenda kwa ajili ya kutajwa tu.

Naibu Msajili huyo alisema jaji atakayepangwa kusikiliza rufani hiyo dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP), atajulikana siku iliyopangwa ya kuanza kusikiliza, ambayo ni leo.

"Ninaahirisha kesi hii ya rufani hadi Februari 14, mwakani na siku hiyo kesi itaanza kusikilizwa mfululizo na Jaji atajulikana siku ya kuanza kwa kusikiliza shauri hilo," alisema.

Mbali na Ole Sabaya washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu na Daniel Mbura na walikuwa wakikabiliwa na mashtaka matatu ya unyang'anyi kwa kutumia silaha.

Oktoba 15, mwaka 2021, wakati akitoa hukumu hiyo, hakimu Amworo, alisema kutokana na ushahidi uliotolewa mahakamani, imewatia hatiani na kuwahukumu miaka 30 kwenda jela kwa kutenda makosa matatu.

Alisema kosa la kwanza na la pili ni la unyang'anyi wa makundi pasipo kutumia silaha, na kosa hilo, lilifanywa na mashtakiwa wote kwa pamoja waliwatendea Numan Yasin na Ramadhani Rashi (mashahidi wa Jamhuri), katika duka la Mohame Saad lililoko Mtaa wa Bondeni jijini Arusha.

Kosa la tatu ni la unyang'anyi wa kutumia silaha ambalo washtakiwa hao, walimtendea Bakari Msangi, walimpiga, kumfunga pingu, kumtishia silaha na kumpora fedha.




Mwakilishi wa Ofisi ya Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) Kanda ya Kusini, akikata utepe kuzindua rasmi matumizi ya thamani za ofisi ambazo ni viti 30 pamoja na meza tano zilizotolewa msaada na TFS kwa ajili ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Masasi (FDC), jana. **PICHA: HAMISI NASRI**

# Wadau mabadiliko ya tabianchi wakunwa sera mpya mazingira

**Na Jenifer Gilla**

JUMAMOSI Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alizindua Sera mpya ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 jijini Dodoma.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mary Maganga, akizungumzia sera hiyo, alisema inaongeza wigo wa kushughulikia masuala na changamoto za mazingira zinazopaswa kufanyiwa kazi katika kipindi husika ili kuleta maendeleo endelevu.

Ofisa Mazingira Mwandamizi kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Fredrick Mulinda, alisema taasisi yao ilikuwa ni moja ya wadau walioshiriki katika kuboresha sera hiyo na kikubwa kilichofanyika ni kuongeza vipengele muhimu vya kushughulikia katika mazingira ili viendane na kasi ya mabadiliko ya kimazingira iliyoko sasa.

"Sera mpya imejumuisha masuala ya mazingira yaliyokuwamo katika sera ya mwaka 1977 na kuongeza mapya sita yakiwamo udhibiti wa taka za kielektroniki, uchafuzi katika shughuli za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, usimamizi wa matumizi ya kemikali, mabadiliko ya tabia nchi, udhibiti viumbe hai na usimamizi wa matumizi salama ya bioteknolojia ya kisasa" alisema Mulinda.

Kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi Mulinda alisema sera hiyo inaongelea hali halisi ilivyo katika nchi na uhitaji uliopo wa mwongozo wa kushughulikia suala hilo ili kuwezesha taifa kujenga uhimili wa mabadiliko hayo.

Mdau wa mazingira na Mkurugenzi wa Lady's Shine Tanzania, Anita Kabwe, alipongeza uamuzi wa serikali wa kuifanyia mabadiliko sera ya mazingira kwa kuwa ilikuwa imeachwa nyuma na teknolojia ya ukuaji wa kasi wa athari ya mabadiliko ya tabianchi.

"Nimefurahi sana kuona serikali imeboresha sera na kuongeza kipengele cha mabadiliko ya tabia nchi na 3.7 kwa kuwa athari zake zinasambaa ni kubwa na zinasambaa kwa kasi, ukirudi miaka 10 nyuma na sasa utaona hali ya hewa imebadilika sana, joto ni kali, mvua hazitabiriki, hali ya uzalishaji wa chakula imeshuka," alisema Anita.

Naye Salum Kigungo, Mkurugenzi wa Taasisi ya Mazingira Tanzania Cleanup and Conservation Initiative (TCCA), alisema amefurahishwa kuona sera mpya ya mazingira imesisitiza ushirikiano na sekta binafsi na wadau wa mazingira katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

"Kifungu namba 3.7 (iii) kimeongelea kukuza ushirikiano na juhudi za Sekta ya Kibinafsi za Mabadiliko ya Tabianchi, hii imenifurahisha zaidi kwa kuwa hapo mwanzo hapakuwa na fair plan ya kuonyesha ni kwa jinsi gani sisi kama wadau tunaweza kushirikiana na serikali katika kupambana na tatizo hili ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu hasa lile namba 13 la mabadiliko ya tabia nchi," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi inayoshughulika na utunzaji wa mazingira ya HUDEFO, Sarah Pima, alipongeza serikali kujumuisha kundi la wanawake katika usimamizi wa mazingira.

Kipengele namba 3.7 katika sera hiyo pamoja na mambo mengine kinachoongelea kuimarisha uwezo wa kitaasisi na rasilimali watu juu ya mabadiliko ya tabianchi kukuza uelewa wa umma juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi, kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

# MSD kuwaletea ahueni wananchi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

MKURUGENZI wa Idara ya Habari (Maelezo) na Msemaji Mkuu wa Serikali, Gerson Msigwa, amesema kuwa Bohari ya Dawa (MSD) imeingia mkataba na watendaji wa mashine na vitendanishi vya huduma ya kusafisha damu (Dialysis) ili kuleta ahueni kwa wananchi.

Aliyasema hayo jana Mjini Zanzibar akizungumza na waandishi wa habari wakati akitoa taarifa ya Serikali ya Tanzania kuhusu masuala mbalimbali ya kimaendeleo.

Alisema baada ya majadiliano na wazalishaji MSD imeafikiana nao kwa bei ya Sh. 57,000 kwa seti ya moja ya vitendanishi ambayo hapo awali MSD ilikuwa inainunua kwa gharama ya Sh. 185,000.

"Sasa kutokana na kupungua kwa gharama za vitendanishi MSD itaweza kuwasambazia watoa huduma kwa gharama ya Sh. 115,000 kwa seti moja ya huduma iliyokamilika ikiwa imejumuisha gharama zote ikiwamo matengenezo ya mashine na usafiri wa kila kitu hadi katika hospitali husika tofauti na gharama ya awali ya kati ya Sh. 200,000 na Sh. 250,000," alisema.

Alieleza kuwa kwa sasa jumla ya mashine 10 kutoka kwa watengenezaji watatu zimesimikwa katika Hospitali ya Chuo Kikuu Dodoma na zinaendelea vizuri.

Aidha, alisema serikali kupitia wizara ya afya, inatekeleza mpango wa pili wa kuziwezesha hospitali za rufani za mkoa kuanza kutoa huduma hiyo ya Dialysis.

Alisema tayari hospitali 15 zimeshafanyiwa uhakiki wa kuanza kutoa huduma hiyo na wataalamu wapo katika mafunzo ya jinsi ya kutoa huduma hizo na ukarabati wa majengo unaendelea.

Msigwa alisema MSD imeshanunua mashine 16 ambazo zitasimikwa kwenye hospitali za rufani za mikoa na kila hospitali itafungiwa mashine 10 pamoja na mashine moja ya kusafisha maji.

Alieleza kuwa MSD imeajiri wataalamu wa vifaa tiba tisa ambao wamekwishapata mafunzo ya kufunga, kufundisha na kufanyia matengenezo mashine hizo na wataalamu hao watatumika kufunga, kutoa mafunzo na sambamba na kuzifanyia matengenezo.

"Hizi ni habari njema sana kwa Watanzania, kwa sababu mahitaji ya huduma hii yameonekana kuongezeka kwa kasi kubwa, lakini gharama zake zimkuwa kikwazo kwa Watanzania. Na kuna kila dalili kuwa hata hiyo 150,000 huenda ikapungua zaidi kwa kuwa wasambazaji wanaendelea kuzungumza na serikali ili kushusha zaidi," alisema.

HABARI MICHEZO

# ILALA QUEENS YAFUNGUKA KUMFUTA KAZI BEIMBAYA

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa timu ya Ilala Queens, umeeleza sababu ya kumfuta kazi Kocha Mkuu, Twaha Beimbaya, ni kukosa matokeo mazuri kwa timu hiyo katika michezo 10 ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Katika idadi ya michezo 10 waliocheza Ilala Queens, imeshinda mmoja na kutoka sare mitatu huku ikipoteza sita, hivyo kujikusanyia pointi sita na zinazowake nafasi ya pili kutokana mkiani mwa ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, mmiliki wa timu hiyo, Omary Kyoma, alisema mbali na kukosa matokeo mazuri, sababu nyingine ya kuondoolewa kwa kocha huyo ni kutokuwapo kwa maelewano mazuri ndani ya benchi lake la ufundi.

Alisema kitendo cha kocha huyo kutokuwa na maelewano na wenzake ndio sababu ya timu hiyo kupata matokeo mabaya katika michezo yao ya Ligi Kuu.

"Hali iliyofikia imetulazimu kufanya mabadiliko kwenye benchi la ufundi kwa kumwondoa Beimbaya na tukiendelea kutafuta kocha mwingine, timu kwa sasa itakuwa chini ya Omary Mbwezeleni," alisema Kyoma.

Gazeti hili lilimtafuta Beimbaya, ambapo alisema hatambui lolote kuhusu kufutwa kazi kwa sababu yuko Morogoro anamalizia kozi ya ukocha ya Diploma B, CAF.

"Sijui lolote, inawezekana maana sijapewa taarifa, kama ni kweli sawa hii inatokana na kutoridhishwa na matokeo ya timu ikiwa chini yangu.

"Nimeiongoza timu kwenye mechi tano, nimefungwa mechi mbili za ugenini, nimeshinda mechi moja na kutoka sare mbili nyumbani," alifafanua Beimbaya.




Paul Peter akishangilia sambamba na wachezaji wenzake baada ya kuifungia timu yake hat-trick kwenye mechi ya Kombe la FA hatua ya 16-bora dhidi ya Baga Friends ya Bagamoyo iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam jana na Azam FC kushinda 6-0. **MPIGAPICHA WETU**

## Coastal Union katika mtihani mgumu leo

**Na Cheji Bakari, TANGA**

TIMU ya Coastal Union 'Wagosi wa Kaya', leo itashuka katika Uwanja wake wa nyumbani, Mkwakwani kuikaribisha Mtibwa Sugar kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la Shirikisho Azam (ASFC) maarufu FA Cup.

Coastal Union itawakaribisha 'Wanatamtam' hao wa Manungu, Turiani katika mechi hiyo baada ya kuitoa timu ya Top Boys FC kwa mabao 8-1 katika hatua ya 32 bora wakati Mtibwa Sugar yenyewe ikiitupa African Sports nje kwa mikwaju ya penalti 4-2.

Wagosi hao wanakutana na Mtibwa Sugar huku ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa na bao 1-0 katika Uwanja wa Manungu, Turiani kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara msimu huu.

Mbali na kufungwa na Mtibwa Sugar iliyoko nafasi ya 14 baada ya kuvuna alama 12 kwenye mechi 14 za Ligi Kuu, huku Coastal Union ikiwa nafasi ya tisa kwa alama zake 17, pia imepoteza mechi tatu mfululizo katika michezo ya ligi hiyo.

Michezo mingine iliyopoteza ni dhidi ya Yanga katika uwanja wa Mkwakani ambapo ilifungwa mabao 2-0, Namungo ikiifunga bao 1-0 uwanjani hapo kabla ya kuifuata Mtibwa Sugar na kuangukia pua kwa goli 1-0 na kisha kupokea kipigo cha 2-1 dhidi ya ndugu zao, Kagera Sugar katika dimba la Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Coastal Union, Steven Mnguto alisema licha ya kupoteza michezo ya Ligi Kuu Bara, lakini watahakikisha hawakubali tena kufungwa na Mtibwa Sugar.

# Azam, Geita zatangulia robo fainali FA

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya matajiri wa Jiji la Dar es Salaam, Azam FC imefanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup, baada ya kuitoa timu ya Baga FC ya Bagamoyo kuisasambua kwa mabao 6-0.

Akizungumza na gazeti hili Jijini Dar es Salaam jana, Kocha Msaidizi wa klabu hiyo, John Yonatas, alisema amefurahishwa na ushindi huo na kuwapongeza wachezaji wake kwa kiwango bora walichokionyesha.

"Tumefurahi kusonga mbele katika mashindano haya ya Kombe la Shirikisho la Azam licha ya mchezo kuwa na ushindani mkubwa," alisema Yonatas.

Alisema baada ya matokeo hayo, kwa sasa wanasubiri kujua timu watakayocheza nayo hatua ya robo fainali.

"Sasa hivi tunasubiri kujua tunacheza nani hatua ya robo fainali ili kuanza kujipanga," alisema.

Aidha, aliweka wazi baada ya mchezo huo wataendelea kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu ya NBC dhidi ya Biashara United utakaopigwa Februari 22, mwaka huu, katika Uwanja wa Azam Coplex, Dar es Salaam.

Katika mchezo huo mabao ya Azam FC yalifungwa na washambuliaji Mzambia, Justin Zulu kwa penalti dakika ya 15, Paul Peter matatu (hat-trick) dakika za 18, 20 na 44, kiungo Mzambia Paul Katema dakika ya 54 na beki Mghana Daniel Amoah dakika ya 89.

Katika mchezo uliotangulia, Geita Gold walikuwa wa kwanza kwenda Robo Fainali baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Mbuni FC, bao pekee la George Mpole dakika ya tatu Uwanja wa Ushirika mjini Moshi mkoani Kilimanjaro likiwavunja hatua hiyo.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### HAALAND NA MAN CITY
KLABU ya Manchester City iko kwenye nafasi nzuri ya kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21. ***(Football Insider)***

### AZPILICUETA KWENDA BARCA
MLINZI wa Chelsea, Cesar Azpilicueta mwenye umri wa miaka 32, ana mkataba wa kujiunga na Barcelona bure wakati mkataba wake wa sasa utakapomalizika kipindi cha majira ya joto. ***(Sport)***

### CAVANI KUONDOKA UNITED
MCHEZAJI Edinson Cavani anatarajiwa kuondoka Manchester United wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu na mshambuliaji huyo wa Uruguay mwenye umri wa miaka 34, angependelea kutimkia Hispania kuliko kurejea nyumbani Amerika Kusini. ***(Fabrizio Romano)***

### ADIDAS KUISAIDIA REAL HAALAND
DHAMIRA ya Real Madrid ya kumsajili Erling Haaland mwenye miaka 21 huenda ikapewa nguvu na Adidas, ambao wanafikiri kumwakilisha mshambuliaji huyo, baada ya kukamaliza mkataba wake na Nike, Januari. ***(Bild, via Marca)***

### TEN HAG ATAKIWA UNITED
MTENDAJI Mkuu mpya wa Manchester United, Richard Arnold anaunga mkono juhudi za Ralf Rangnick za kumnasa kocha wa Ajax, Erik ten Hag kuwa kocha mpya wa timu hiyo, licha ya wachezaji wengi kumtaka kocha wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino. ***(Sun)***

### FIRMINO KUPEWA MKATABA
LIVERPOOL inatarajia kumpa mkataba mpya mshambuliaji Mbrazil, Roberto Firmino mwenye umri wa miaka 30. ***(Football Insider)***

### RODGERS KUHAMIA MANCHESTER
KOCHA wa Leicester, Brendan Rodgers amezidi kuchochea uvumi kwamba kazi yake ijayo itakuwa kwenye mji wa Manchester, baada ya kutafuta makazi mapya karibu na eneo la soka la Cheshire. ***(Sun)***

### DENAYER ASUBIRIWA LYON
KLABU ya Lyon inaendelea kusubiria majibu ya Jason Denayer mwenye umri wa miaka 26, kama atakubali ofa yao na mkataba mpya, huku Barcelona, Newcastle, Juventus na Napoli wakimfuatilia mlinzi huyo wa Ubelgiji, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Het Nieuwsblad)***

### FEKIR HUYOOO BARCA
BARCELONA wanajiandaa kulipa pauni milioni 50.2 ili kumsajili mshambuliaji wa Ufaransa, Nabil Fekir, ingawa klabu ya zamani ya nyota huyo mwenye umri wa miaka 28, Real Betis inataka pauni milioni 66.2. ***(Sport)***

### ADEYEMI KUTUA DORTMUND
KLABU ya Borussia Dortmund inaamini itafikia makubaliano ya kumsajili mshambuliaji wa Ujerumani, Karim Adeyemi mwenye umri wa miaka 20, kwa mkataba wa miaka mitano kutoka Red Bull Salzburg. ***(Fabrizio Romano)***

### SOMONS MKATABA MPYA
KLABU ya Paris St-Germain haina shaka na iko tayari kumpa kiungo Mholanzi Xavi Simons mwenye umri wa miaka 18, mkataba mpya kabla ule wa sasa kumalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Mundo Deportivo)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# TUCHEL APAGAWA CHELSEA KUBEBA KOMBE LA DUNIA

Sote tuna ndoto ya kuwa na fainali kama hizi, bado kuna mambo ya kushinda na haikomi...

**DOHA, Qatar**

THOMAS Tuchel amesema Chelsea ilistahili ushindi wa Klabu Bingwa Dunia na ametoa changamoto kwa timu yake "isiyochoka" kuendelea kuongeza mkusanyiko wao wa mataji katika kipindi kilichosalia cha msimu.

Kai Havertz alifunga penalti ya muda wa ziada na kupata ushindi wa 2-1 dhidi ya mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini, Copa Libertadores, Palmeiras.

Tuchel, ambaye hakuwapo benchi kwenye ushindi wa nusu fainali ya timu yake dhidi ya Al Hilal baada ya kukutwa na COVID-19, lakini akaweza kusafiri hadi Falme za Kiarabu kwa fainali hiyo.

Huku akikiri kwamba Chelsea ilihitaji bahati kidogo ili kuepuka mikwaju ya penalti, bosi huyo wa zamani wa Paris Saint-German aliona kuwa huo ni ushindi waliostahili.

"Unahitaji bahati ili kupata bao la kuchelewa, lakini hatukuchoka, na hatukuacha kujaribu", alisema Tuchel akiiambia Channel 4, baada ya kuona bao la kwanza la Romelu Lukaku likisawazishwa kwa mkwaju wa penalti na Raphael Veiga.

"Hatukukubali. Tulikuwa na bao la kuongoza, kisha tukapoteza, lakini hatukusimama. Tulistahili, lakini ni bahati unapopata bao kwa kuchelewa.

"Penalti (kutoka kwa Havertz) haikuonekana kuwa na wasiwasi, lakini kwa hakika alikuwa imara

"Huwezi kuwa na wasiwasi katika hali hii. Tuliamini takwimu, na nina furaha kwa ajili yake."

Kwa mkwaju wake wa mafanikio, Havertz amekuwa mchezaji wa kwanza kufunga bao la ushindi katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Klabu Bingwa Dunia tangu Lionel Messi alipofanya hivyo mwaka 2011.

Ingawa Tuchel alikuwa na hamu ya kufurahia taji la kwanza la dunia la Chelsea, alisisitiza kwamba bado kuna mengi ya kukamilisha pale Stamford Bridge.

"Ninaweza kuwa sehemu yake (kushinda mataji) na nina furaha kupata nafasi. Tulisema hapo awali kwenye chumba cha kubadilishia nguo 'ni fursa gani'," alisema.

"Sote tuna ndoto ya kuwa na fainali kama hizi. Hakuna majuto. Bado kuna mambo ya kushinda, na haikomi."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MALLORCA
VERSUS
ATHLETIC BILBAO
1 | 3.30
X | 3.05
2 | 2.33

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# KLOPP: SALAH ATASAINI MKATABA MPYA LIVER



**LIVERPOOL, England**

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amedokeza kwamba, ana matumaini ya suala la mkataba mpya la Mohamed Salah litafikia suluhisho, huku akisema wachezaji wanaofikia umri wa miaka 30, wanakuwa kwenye kiwango chao bora zaidi.

Salah, ambaye anatimiza umri wa miaka 30 Juni mwaka huu, amebakiwa na miezi 18 katika mkataba wake wa sasa na Liverpool, lakini mazungumzo yanaendelea kuhusu mkataba mpya.

Nyota huyo wa kimataifa wa Misri aliwahi kudokeza kwamba anataka kubaki Liverpool ingawa kulikuwa na ripoti kwamba wawakilishi wake wanataka dili la mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki.

Wamiliki wa Liverpool, Fenway Sports Group wamekuwa wakisita kutoa mkataba mnono kwa wachezaji ambao wanafikia umri wa miaka 30.

"Mwaka mmoja au miwili iliyopita wachezaji watatu wa mwanzo wa Ballon d'Or, pamoja na Salah ambaye alikuwa mdogo zaidi, wote walikuwa wakubwa wenye umri wa miaka 34 au zaidi," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari kuelekea mchezo wa jana Jumapili dhidi ya Burnley.

"Lewandowski ana miaka 33, halafu Messi na Ronaldo wana 34 na 37 na kama una bahati zaidi ya kucheza bila ya kupata majeraha, unaweza kucheza kwa muda mrefu zaidi.

"Naamini suala la Salah litafikiwa tu makubaliano."

# Scholes amkataa Rangnick United

**MANCHESTER, England**

PAUL Scholes anaamini, Ralf Rangnick sio kocha sahihi wa Manchester United, ambao kiwango chao kibaya kiliendelea dhidi ya Southampton Jumamosi.

United walitoka sare mechi ya pili mfululizo ya Ligi Kuu baada ya Che Adams kufuta bao la kwanza la Jadon Sancho kwenye Uwanja wa Old Trafford.

'Mashetani Wekundu' hao walishikiliwa na Burnley katikati ya wiki, ambayo ilitokana na kushindwa kwa mikwaju ya penalti na Middlesbrough kwenye Kombe la FA mnamo Februari 4, mwaka huu.

United waliongoza hadi mapumziko katika mechi zote tatu, huku sare hizo mbili za Ligi Kuu ikiwa ni mara ya pili tu katika historia ya mashindano hayo kushindwa kushinda mechi mfululizo baada ya kuwa mbele wakati wa mapumziko.

United inashika nafasi ya tano na imewapa wapinzani wao nafasi ya kusonga mbele katika mbio za kufuzu kwa Ligi ya Mabingwa Ulaya.



Rangnick alichukua nafasi ya Ole Gunnar Solskjaer Novemba kwa muda hadi mwisho wa msimu, huku kocha huyo wa zamani wa RB Leipzig na mkurugenzi pia akitarajiwa kuchukua jukumu la ushauri hadi 2024.

Hata hivyo, United ina wastani wa mabao machache kwa kila mechi chini ya Rangnick kuliko ilivyokuwa chini ya kocha mwingine yeyote katika historia ya Ligi Kuu England.

Na nyota wa zamani wa United Scholes hajafurahishwa na kile alichokiona hadi sasa.

"Hiyo ndiyo hisia ya mahali (tulivu ndani ya Old Trafford) kuna ukosefu wa nia sasa na jinsi msimu ulivyokuwa," alisema Scholes akiiambia BT Sport.

"Imekuwa siku saba mbaya, kwa kweli imekuwa miezi sita au saba mbaya.

"Kufukuzwa kwa Ole kunakuja, sote tulijua hilo, lakini mpango ulikuwa wapi? Lazima kuwe na mpango, lazima kuwe na wasomi, kocha wa juu katika klabu ya soka.

"Na Manchester United, wanapaswa kuwa na kila kitu bora zaidi, na kutokuwa na mpango na kuleta kile ambacho ni mkurugenzi wa michezo ... amefundisha timu kwa miaka miwili kati ya 10 iliyopita.

"Usinielewe vibaya, napenda mtu, anakuja vizuri, lakini ameonekana kukosa kufundisha katika kipindi cha miaka mitano au sita iliyopita.

"Timu moja ina kocha mzuri, timu nyingine ina mkurugenzi wa michezo, jambo ambalo si sahihi kwa Manchester United."

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# YONDANI ATAJWA SABABU VIPIGO KWA POLISI TANZANIA

**Na Adam Fungamwango**

KUHAMA kwa baadhi ya wachezaji wa Polisi Tanzania kipindi cha dirisha dogo akiwamo beki Kelvin Yondani, kumetajwa kuwa ni sababu ya timu hiyo kufanya vibaya kwa sasa.

Wakizungumza hayo kwenye mazoezi ya timu hiyo, mashabiki wa timu hiyo wamedai kuondoka kwa wachezaji kadhaa muhimu ndiko kulikosababisha timu hiyo kuwa na mwendo mbaya kwa sasa, huku baadhi ya wachezaji wakikosa utimamu wa mwili.

"Utimamu wa mwili walioanza nao wachezaji ni tofauti na sasa, mwanzoni walikuwa vizuri wakati ligi inaanza, lakini naona kila mechi zinavyozidi kusonga mbele, wachezaji wanakosa nguvu," alisema Athumani Sinundo shabiki wa timu hiyo mkoani Kilimanjaro.

Shabiki mwingine Haji Michael, alisema klabu ilishindwa kuwabakisha wachezaji muhimu kwa kuwaongezea mikataba, akiwamo Yondani, hivyo pengo lake na wengine ndilo linalowaathiri kwa sasa.

"Alipokuwapo Yondani, ulinzi kule nyuma ulikuwa madhubuti, lakini baada ya kuondoka unaona kule nyuma kulivyo?" Alilalamika.

Polisi Tanzania haijashinda mechi sita mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara, huku mara ya mwisho kushinda ikiwa ni Desemba 4, mwaka jana ilipoifunga Prisons bao 1-0.

Kati ya mechi hizo sita mfululizo ambazo imeshindwa kupata ushindi, imetoka sare nne na kupoteza mechi mbili mfululizo ikifungwa bao 1-0 dhidi ya Yanga Januari 23 na Februari 6 ikichapwa mabao 3-1 dhidi ya Geita Gold.

Iko kwenye nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi, ikiwa na pointi 18 kwa mechi 14 ilizocheza.


Kelvin Yondani

# Dodoma Jiji yainolea makali Pamba FA Cup

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Dodoma Jiji imesema iko imara na tayari kukutana na timu ya Pamba FC ya Mwanza kwenye mchezo wa hatua ya 16-bora wa Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup utakaopigwa Jumatano wiki hii.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa klabu hiyo, Mbwana Makata, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu watakuwa ugenini, lakini watajitahidi kuhakikisha wanapata matokeo.

"Tunaendelea na maandalizi ya mchezo wetu huo, tunaamini utakuwa mgumu na wenye ushindani mkubwa, lakini tumejipanga," alisema Makata.

Kocha huyo alisema anauheshimu mchezo huo kwa kuwa katika mashindano hayo timu zote zimejipanga vizuri hasa ukizingatia inayofungwa


Mbwana Makata

inatoka mashindanoni.

Aliongeza mikakati yao ni kushinda mchezo huo na kuingia kwenye hatua ya robo fainali, hivyo hatakuwa tayari kufanya makosa.

Alisema kikubwa anachofanya mbali na mazoezi ya kila siku ni kuendelea kuwajenga wachezaji wake kisaikolojia pamoja na kurekebisha makosa madogo madogo ambayo ameyabaini kwenye michezo iliyopita.

Kuhusu hali za wachezaji kiafya, alisema wanaendelea vizuri isipokuwa mchezaji Steven Mganga, ambaye anasumbuliwa na goti.

Aliomba mashabiki wa timu hiyo kuendelea kuwaunga mkono ili wafike mbali na kuzidi kulitangaza Jiji lao la Dodoma.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 14/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 4265 | Persepam MU vs Persiraja Banda | 1.38 | 4.34 | 6.94 |
| 15:00 | 2726 | Spartak Subotica vs Radnik Surduluca | 1.96 | 3.32 | 3.46 |
| 16:00 | 3324 | El Ittihad Alexandria vs Eastern Company SC | 1.46 | 4.14 | 6.71 |
| 16:00 | 5112 | AL Khlood vs Al Khaleej Club | 3.23 | 2.99 | 2.19 |
| 16:05 | 4390 | Najran SC vs Hajer Club | 2.46 | 2.79 | 2.99 |
| 16:55 | 4663 | East Riffa vs Najma Manama | 1.45 | 4.32 | 5.57 |
| 17:00 | 1531 | Ruzomberok vs MSK Zilina | 2.36 | 3.36 | 2.64 |
| 17:00 | 3597 | Kerala Blasters FC vs East Bengal | 1.60 | 3.86 | 4.63 |
| 17:00 | 4825 | Vojvodina vs FK Napredak | 1.56 | 3.85 | 5.01 |
| 18:10 | 1355 | AL Jeel vs AL Adalh | 2.51 | 2.85 | 2.85 |
| 18:15 | 1091 | Persebaya Surabaya vs Persija Jakarta | 2.44 | 3.02 | 2.78 |
| 18:30 | 5931 | Botosani vs Clinceni | 1.16 | 6.49 | 15.73 |
| 18:45 | 2033 | Din. Tirana vs Laci | 3.67 | 2.80 | 2.13 |
| 18:45 | 5918 | Skenderbeu vs Partizani Tirana | 4.90 | 3.10 | 1.87 |
| 19:00 | 4645 | Anorthosis Famagusta vs Olympiakos Nicosia | 1.53 | 3.86 | 6.33 |
| 19:30 | 2567 | NK Aluminij vs NK Radomlje | 2.13 | 3.27 | 3.08 |
| 19:30 | 4331 | AL Khalidiyah vs Riffa Club | 3.42 | 3.37 | 1.96 |
| 20:00 | 1068 | Adana Demirspor vs Besiktas | 2.40 | 3.31 | 2.81 |
| 20:00 | 3547 | Hatayspor vs Goeztepe | 2.46 | 3.20 | 2.81 |
| 20:00 | 4166 | Gornik Zabrze vs Jagiellonia | 2.03 | 3.37 | 3.22 |
| 20:30 | 2670 | PAS Giannina vs Aris Salonica | 2.85 | 3.00 | 2.56 |
| 20:30 | 4499 | Hull City U23 vs Barnsley U23 | 1.89 | 3.97 | 3.14 |
| 20:30 | 5454 | Baroka FC vs Mamelodi Sundowns | 11.76 | 4.90 | 1.26 |
| 20:45 | 1823 | Orleans vs Red Star | 2.45 | 3.08 | 2.84 |
| 20:55 | 4254 | Universitatea Craiova vs U Craiova SA | 1.60 | 3.58 | 5.69 |
| 21:00 | 1727 | Rio Ave vs CF Estrela | 1.58 | 3.81 | 5.27 |
| 21:00 | 3551 | Viktoria Koln vs Osnabruck | 2.90 | 3.30 | 2.31 |
| 21:00 | 5690 | GD Chaves vs Vilafranquense | 1.78 | 3.48 | 4.22 |
| 21:00 | 5717 | Misr Lel Makasa vs Talaea El Gaish | 3.01 | 2.96 | 2.47 |
| 21:15 | 1206 | Ironi Kiryat Shmona vs Maccabi Haifa | 7.90 | 4.63 | 1.32 |
| 21:15 | 4901 | Apoel Nicosia vs AEK Larnaca | 2.27 | 3.13 | 3.23 |
| 21:30 | 2225 | Zulte Waregem U21 vs Anderlecht U21 | 7.71 | 5.59 | 1.26 |
| 21:30 | 3814 | Mouscron U21 vs AS Eupen U21 | 3.37 | 3.66 | 1.89 |
| 21:30 | 4837 | Antwerp U21 vs Charleroi U21 | 3.25 | 3.65 | 2.09 |
| 21:30 | 4918 | Kortrijk U21 vs Union Saint Gilloise U21 | 3.18 | 3.86 | 1.90 |
| 21:30 | 5497 | KRC Genk U21 vs Mechelen U21 | 1.08 | 8.84 | 17.30 |
| 21:45 | 2707 | KF Tirana vs Egnatia Rrogozhine | 1.28 | 4.72 | 9.25 |
| 22:00 | 3532 | Westerlo U21 vs Lommel U21 | 1.50 | 4.44 | 4.83 |
| 22:00 | 4942 | Kecskemeti TE vs Diosgyori Vtk | 2.55 | 3.23 | 2.51 |
| 22:00 | 5527 | Kmsk Deinze U21 vs Waasland Beveren U21 | 3.23 | 3.95 | 1.86 |
| 22:00 | 5576 | Jong PSV vs Jong Utrecht | 1.64 | 4.02 | 4.42 |
| 22:45 | 1193 | Le Havre vs Bastia | 2.54 | 2.89 | 2.94 |
| 22:45 | 1967 | Spezia vs Fiorentina | 3.80 | 3.70 | 1.90 |
| 22:45 | 2968 | Peterhead vs Dundee FC | 4.84 | 3.68 | 1.61 |
| 23:00 | 2083 | AC Reggiana vs Pescara Calcio | 1.70 | 3.61 | 4.85 |
| 23:00 | 4048 | Ponferradina vs Real Sociedad B | 1.86 | 3.29 | 4.22 |
| 23:00 | 4131 | Orsomarso vs Universitario Popayan | 1.69 | 3.46 | 4.52 |
| 23:00 | 4752 | West Bromwich vs Blackburn | 1.82 | 3.42 | 4.20 |
| 23:00 | 5834 | Mallorca vs Athletic Bilbao | 3.30 | 3.05 | 2.33 |
| 23:15 | 4455 | FC Arouca vs Maritimo | 2.46 | 3.15 | 2.85 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatatu Februari 14, 2022
Nipashe

UKURASA 21



**Tuchel apagawa Chelsea kubeba Kombe la Dunia**

WAYA...




Kiungo mshambuliaji wa Simba, Pape Sakho, akibinjuka na kuifungia timu yake bao la kwanza wakati ikishinda 3-1 dhidi ya Asec Mimosas kwenye mechi ya hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA YAANZA KWA KUKAA KILELENI CAF

●●●Bocco arejesha makali Sakho akifunga bao la mwaka huku Banda akifanya yake kwa Asec Mimosas....

**Na Adam Fungamwango**

MABAO mawili ya haraka haraka yaliyofungwa ndani ya dakika tatu na Shomari Kapombe kwa mkwaju wa penalti pia winga chipukizi raia wa Malawi, Peter Banda, yaliiwezesha Simba kuanza vema michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika hatua ya makundi kwa kuichapa Asec Misosas ya Ivory Coastal 3-1 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na kukaa kileleni mwa Kundi D.

Mabadiliko mawili yaliyofanywa na Kocha Mkuu Pablo Franco kwa kuwatoa Meddie Kagere na Sadio Kanoute, akiwaingiza nahodha John Bocco na Yusuph Mhilu dakika ya 70, ndiyo yaliyochagiza kwa kiasi kikubwa timu hiyo kuibuka na ushindi huo.

Wakati ikionekana kama Asec Mimosas ikitaka sare huku ikiutawala mchezo, mpira wa krosi uliopigwa na Bocco ulizua kizaazaa kwenye lango la wageni na kusababisha kipa Abdulkarim Cisse kumkamata mguu Mhilu na kuzaa penalti ambayo wachezaji wa Simba walionekana kuogopa kwenda kupiga wakikumbuka 'mzimu' wao wa kukosa penalti nyingi kwenye Ligi Kuu na michuano ya kimataifa.

Beki wa kulia Kapombe alijitoa mhanga na kupiga penalti kwa ufundi, iliyokwenda wavuni na kuandika bao la pili dakika ya 77.

Shambulio lingine la kushtukiza lililofanywa na Simba liliiwezesha kupata bao la tatu, baada ya Bocco tena ambaye alikuwa katika kiwango cha juu jana, kupata mpira mrefu kulia mwa uwanja, akiwazidi mbio mabeki wa Asec Mimosas na kupiga krosi ya nyuma, iliyomkuta Banda akiwa kwenye mbio, bila kutuliza akaujaza wavuni dakika ya 80 na kuandika bao la tatu.

Ilikuwa ni ahueni kwake, kwani aliikosesha Simba bao la wazi dakika ya 44, akiwa amebaki yeye na kipa Cisse, na ilikuwa vigumu zaidi kukosa kuliko kupata, kiasi cha kuudokoa tu, lakini alipiga shuti kubwa mpira ukapaa juu kwa mshangao wa wengi.

Ilikuwa ni hoi hoi nderemo na vifijo kwa viongozi, wanachama na mashabiki wa Simba waliokuwa uwanjani na hata ambao walikuwa kimya wakisononeka, tangu lilipofungwa bao la kusawazisha dakika ya 52 na Stephane Aziz Ki.

Kiungo huyo raia wa Burkina Faso alipata mpira uliombabua mchezaji mwenzake, kutokana na makosa ya Onyago aliyetaka kupiga mbele, lakini ulirudi tena golini kwake, baada ya tukio hilo na kumkuta mfungaji aliyemzunguka Henoc Inonga na kuujaza wavuni.

Shambulio la kwanza la hatari ndilo lililozaa bao la kwanza kwa Simba dakika ya 12, baada ya Msenegal Pape Sakho alipowainua vitini mashabiki wa Simba waliokuwa uwanjani.

Ilikuwa ni krosi ya shomari Kapombe ilionekana kama haikuwa hatari sana, lakini Sakho kwa ustadi wa hali ya juu, alibinjuka na kupiga 'tik-tak' safi na mpira kujaa wavuni, akimwacha kipa Abdulkarim Cisse asijue la kufanya.

Kuingia kwa bao hilo kulionekana kuwaamsha Asec Mimosas na pia kuwafanya Simba kupooza na kuwaacha wageni kutawala soka kwa muda.

Dakika nne baada ya Simba kufunga bao, nusura Asec Mimosas wasawazishe, pale Anicet Oura alipoupata mpira umbali wa mita 35, akimvizia Aishi Manula akiwa ametoka kidogo langoni, lakini shuti lake lilipaa juu.

Simba ingeweza kuhesabu bao la pili dakika ya 22, pale straika wake Meddie Kagere alipotengewa mpira na Peter Banda, lakini alipiga mpira uliogonga nguzo ya pembeni ya goli, kabla ya kurejea uwanjani.

Uzembe wa mabeki na viungo wakabaji wa Simba ulimfanya Karim Konate kubaki na kipa Manula dakika ya 37, lakini kwa bahati shuti lake lilidakwa kwa ustadi na kipa Manula.

Sakho ambaye alikuwa hatari zaidi kwa mabeki wa Asec Mimosas ilibidi atolewe kipindi cha kwanza baada ya kuumia, licha ya juhudi za kutaka aendelee na nafasi yake kuchukuliwa na Mzamiri Yassin.

Kwa matokeo hayo Simba iliyo kwenye Kundi D, imevuna pointi tatu na mabao matatu na kuiweka njia yake vema ya kuisaka robo fainali ya michuano hiyo.

## Yanga na hesabu kali kwa Biashara

**Na Saada Akida**

KOCHA wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesema wataingia katika mchezo wa hatua ya 16-bora dhidi ya Biashara United kwa tahadhari kubwa kwani utatoa taswira ya wao kuendelea hatua inayofuata.

Yanga inashuka kwenye mechi hiyo ikiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa mabao 2-1, mchezo wa mwisho waliokutana Ligi Kuu Tanzania Bara ambao uliopigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Yanga ilitinga hatua ya 16-bora baada ya kuiondosha mashindanoni Mbao FC, kwa kuichapa bao 1-0, mchezo uliopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi, alisema kila kitu kuelekea mchezo huo kimekamilika ingawa bado anaenda kuwakosa baadhi ya wachezaji wake muhimu Dickson Job na Shaban Djuma kutokana na adhabu.

"Tutaingia kwa tahadhari kubwa, Biashara United ni timu nzuri ambayo kama tutafanya uzembe tunaweza kupoteza, sitaki hili litokee," alisema Nabi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >